# MIONGONI MWA ITIKADI ZA SHIA

MTUNZI

ABDALLAH BIN MUHAMMED AS-SALAFY

*UTANGULIZI WA SHEIKH ABDUL-AZIZ BIN ABDALLAH BIN BAAZI KIONGOZI WA JOPO LA WANAZUONI WAKUU WA SAUDI ARABIA*

*Kwa jina la Mwenywezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu.*

Kutoka kwa Abdul-azizi bin Adballah bin Bazzi, kwa ndugu yangu mkarimu….Allah amuafikishe.

Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yako na rehma zake pamoja na baraka zake,amma baad:

Kutokana na barua yako ulio ituma kwangu ya tarehe 10/2/1418h kuhusu kitabu chako, juu ya" Shi'a ", tumekisoma, na kukiona kuwa ni kizuri na muhimu sana, kinafaa kuki sambaza hapa saudia na kwingineko, na tunamuomba Allah awanufaishe kwacho waislamu na atie baraka katika juhudi zenu.

Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu na rehema pamoja na baraka zake.

Mufti wa Saudi-arabia.

## *UTANGULIZI*

Shukurani zote zinamstahiki Allah peke yake,Rehma na amani zimwendee Mtume(s.w.a) pamoja na ahli zake na swahaba wake wote. Amma baad:

Hakika sababu za msingi zilizo nipelekea kuandika ki tabu hiki na hali iliyo jionyesha ya kushamiri kwa harakati za Raafidhwa za kuwalingania watu katika dhehebu hili potofu na harakati hizi zimekuwa kiulimwengu, na kutokana na hatari kubwa ya kundi hili kwa dini ya uislamu na kutokana na hali ya kughafilika na kuji sahau kwa waislamu wengi kutokana na hatari ya kundi hili, na kutokana na itikadi yao iliyo jaa ushirikina, na kuitukana Qur-an na Maswahaba-Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao-na kupituka mipaka juu ya Maimamu wao, ndio maana nimeazimia kuandikakitabu hiki na kuyajibu mambo yanayo watatiza watu kuhusu kundi hili kwa muhtasari, nikufuata nyayo za Sheikh wetu Sheikh Abdallah bin Abdurahman-aljibrin- Mungu amuhifadhi-katika kitabu chake "Atlaaliiqaat alaa Matni lumuatil-iitiqaad" na kwa kunukuu katika vitabu vya Raafidhwa ambavyo ni maaraufu na mashuhuri kwao, na katika vya Ahlusuna miongoni mwa wema walio tangulia na walio kuja baaada yao amabao waliwajibu Raafidhwa na kubainisha ubovu wa itikadi zao zilizo simama juu ya ushirikina, na uongo, na kuchupa mipaka, na matusi.

Na nimejaribu kwa kadri ya uwezo wangu katika kitabu hiki kuwasimamishia hoja,kupitia vitabu vyao wanavyo vitegemea, kama alivyo sema Sheikh Ibrahim bin Sulaiman Aljab-han-Mwenyezi Mungu amrehem-"Nitakusimamishia hojakupitia mdomowako ewe Shi'a.

Mwisho na muomba Allah awanufaishekupitia kitabu hiki wenye mazingatio kama alivyo sema Allah "*Hakika katika hayo mna ukumbusho kwa wenye kuwa na nyoyo zinazo zingatia, aumwenye kutega sikio na hali moyo wake uko hadhir*" Qaf:37

Natoa shukrani kwa kila alie changia katika kitabu hiki,namuomba Allah awalipe kila la kheri.

Rehma na amani zimuendee bwana wetu Muhammad na ahli zake na Maswahaba zake.

Imeandikwa na Abdallah Muhammad Assalafy.

## *NI LINI LIMEDHIHIRI KUNDI LA RAAFIDHWA?*

Lili anza kundi la Raafidhwa wakati alipojitokeza Myahudi mmoja aitwae (Abdallah bin sabai) akidai kuwa ni Muislam, na kwa madai ya kuwapenda Ahlul bayt (watu wa nyumbani kwa Mtume) na akapituka mipaka katika kumtukuza Ally (r.a) na akadai kuwa mtume alimuusia kuwa khalifa baada yake, kisha akamnyanyua na kumuweka katika daraja ya uungu na haya yanathibitishwa na vitabu vya kishia.

Kwa mfano Alqmmy katika kitabu chake (Almqaalatu walfiraq) (1): Anakiri kuwepo kwake (Ibnu sabai) na anamzingatia kwamba ndie mtu wa mwanzo aliesema kuhusiana na uimamu wa Ally na kurejea kwake, na akaanzisha kuwatukana Abubakari na Omar na Uthmani na maswahaba wengine, kama alivyosema Annuubkhty katika kitabu chake (Firaq Shia) (2). Nakama alivyosema pia Alkushiy katika kitabuchake maarufu ( Rijaalul-kushiy) (3). Na katika mashia wa sasa hivi wanaosema kuwepo kwa Abdalla bin Sabai ni Muhammad bin Ally Al muallim katika kitabu chake ( Abdallah bi Sabai Alhaqiikatul-majuhuula) (4). Na mtu kukubali jambo ndio dalili kubwa, nahawa wote tulio wataja ni katika Mashekhe wakubwa wa kiraafidhwa.

Amesema Albaghdaadiy: "Assabaiyya ni wafuasi wa Abdallah bin Sabai ambae alichupa mipaka katika kumtukuza Ally (r.a) na kudai kuwa alikuwa ni Nabii, Kisha akachupa mipaka zaidi mpaka akadai kuwa alikuwa ni Mungu".

Na amesema Albaghdaadiy vilevile: "Na alikuwa Ibnu Saudai- yaani Ibnu Sabai- Asili yake ni Myahudi katika watu wa Aliirah, akadhihirisha Uislamu kwa kutaka awena ukubwa kwa watu wa Alkuufa, akawaambia(watu wa kuufa) kwamba amekuta katika Taurati kwamba kila Mtume anae waswiy (mrithi) na kwamba Ally (r.a) ndie mrithi wa Mtume (s.a.w)".

Na amesema Ashihristany kuhusu Ibni Sabai kwamba ndie mtu wa kwanza aliesema kwamba kuna nasswi (dalili) juu ya uimamu wa Ally (r.a), na akaeleza kuhusu kundi la Sabaiya kwamba ndilo kundi la kwanza lililo anzisha itikadi ya kutoweka kwa Imamu wao wa kumi na mbili(Almahd Almuntadhwar) na kurejea kwake, kisha Shia wakarithi itikadi hiyo baada yao, pamoja na kutofautiana kwa makundi yao,kuhusu uimamu wa Ally na ukhalifa wake. Na hayo ni katika athari za Ibni Sabai, na yaliongezeka makundi ya Shia na itikadi zao na kauli zao yakawa makundi mengi sana.

Nahivi ndivyo walivyo zua Mashia itikadi ya Alwaswiy, Arrajaa, Alghaiba, bali itikadi ya kwamba maimamu wao wanasifa za uungu (5) kwa kumfuata Myahudi Ibnu sabai.

(1) Rejea: Almaqaalaatu wal firaq cha Alqummy uk.10-21
(2) Rejea: Firaqu Shia cha Anuubakhty uk. 19-20
(3) Rejea: aliyoyataja Alkushiy katika riwaya zake mbalimbali kutoka kwa Ibni Sabai na itikadi zake, tazama namba: 170,171,172,173,174 katika uk. 106-108
(4) Na kitabu hiki ni majibu ya kitabu alichokitunga mshia aitwae Murtadhwa Al-askary kwa anuani (Abdallah bin Sabai wa asaatwiru ukhra) ambae alipinga katika kitabu chake kuwepo kwa Abdallah bin Sabai.
(5) Rejea Usuulu i-itiqaad Ahli Sunna waljamaa cha Allaalakaaiy (1/22-23).

*KWANINI SHIA WAMEITWA RAAFIDHWA?*

Jina hili kalitaja Sheikh wao Almajlisy katika kitabu chake (Bihaarul-anwar) akasema katika mlango alio uita, mlango kuhusu ( Ubora wa raafidhwa na uzuri wa kujiita jina hili), kisha akataja kutoka kwa Sulaiman Al-aamash kuwa amesema: niliingia kwa Abii Abdillah Jaafar bin Muhammad nikasema kumwambia: Hakika watu wanatuita Raafidhwa, nini maana ya Raafidhwa? Akasema: wallahi sio wao walio kuiteni hivyo bali Mwenyezi Mungu alikuiteni hivyo katika Taurati na Injili kupitia ulimi wa nabii Mussa na nabii Issa. (1)

Na imesemekana kuwa: wameitwa raafidhwa kwa sababu walikuja kwa Ally bi Hassan wakamwambia: Jitenge na Abubakari na Omar ili tuwe pamoja nawe, akasema: wao ni vipenzi wa Babu yangu, siwezi kujitenga nao bali niko pamoja nao, wakasema: hivyo basi tumekukataa, ndipo wakaitwa Raafidhwa, na akaitwa kila alie muunga mkono Zaid kuwa ni Zaydiyya. (2)

Na inasemekana:wameitwa Raafidhwa kwa kupinga kwao utawala wa Abubakari na Omar. (3)

Na imesemekana: Wameitwa hivyo kwa kukataa kwao Dini. (4)

(1) Tazama kitabu (Bihaarul-anwar) cha Almajlisy 65/97. (ambacho ni miongoni mwa marejeo yao muhimu katika vitabu vyao vya sasa)
(2) Rejea: Attaaliqaat alaa matni lum-atul iitqaad cha Sheikh Abdallah Aljibriin uk.108.
(3) Tazama Maqaalaatul-Islaamiyiin cha muhyi ddiin Abdulhamiid (1/89)
(4) Maqaalatul Islamiyiin 1/89

## *RAAFIDHWA WAMEGAWANYIKA MAKUNDI MANGAPI?*

Imekuja katika kitabu (Daairatul-maarif) kuwa "Makundi ya Shia ambayo ni mashuhuru yako zaidi ya sabini na tatu"(1)

Bali imepokewa kutoka kwa Raafidhwa Mir baaqir Addaamand (2) kwamba makundi yote yaliyotajjwa katika Hadithi, Hadithi ya kugawanyika kwa Umma wa Muhammad katika makundi sabini na tatu yamekusudiwa makundi ya Mashia, na kwamba lililotajwa kuwa ni kundi lililosalimika ni kundi la imaamiyya.

Na ametaja Almaqriizy kuwa makundi yao yanafikia mia tatu .
Na amesema Ashihristany: "Hakika Raafidhwa wamegawanyika katika makundi matano:Alqiisaaniyya, Azaydiyya, Al imaamiyya, Alghaaliyya, Al ismaailiyya," (4)

Na amesema Albaghdaady: " Hakika Raafidhwa baada ya zama za Ally (r.a) wako makundi manne: Zaidiyya, Imaamiyya, Kiisaaniyya, na Alghulaatu" (5)

Lakini yakupasa kutambua kuwa Zaydiyya si katika kundi la Raafidhwa ispokuwa kundi la Aljaaruudiyya.

---

(1) Rejea: Daairatul Maarif (4/67)
(2) Ni Baaqir bin Muhammad Al-istiraabaady, Maarufu kama Al-miir Addamaad, amekufa mwaka 1041.Tazama maelezo yake katika kitabu (Alkunaa-wal-alqaab) cha Abbaas Alqummy 2/226
(3) Ni Almaqriizy (2/351)
(4) Rejea: Almilal wannihal cha Ashihristaany uk.147
(5) Rejea: Alfarqu bainal-firaq, cha Albaghdaady uk.41

*NI IPI ITIKADI YA ALBADAA WANAYO IAMINI RAAFIDHWA?*

Al badaa maana yake ni kudhihiri baada ya kutoweka, au kwa maana ya kuanzishwa kwa rai mpya. Na neno hili (Albadaa kwa maana zote mbili linamaanisha kuwepo hali ya kutojua jambo kisha kujua kunakuja baadae, na mambo yote haya mawili kwa Allah ni muhali, aliki Raafidhwa wanainasibisha sifahii ya ( Albadaa) kwa Mwenyezi Mungu.

Imepokewa kutoka kwa Rayyaani bin Asswalt kwamba amesema:" nilimsikia Arridhwaa akisema: hajapata Mwenyezi Mungu kumtuma nabii yoyote ispokuwa kwa kuharamisha pombe na kukiri (Albadaa) kuwa ni katika sifa za Allah" (1)

Na kutoka kwa Abdalla amesema: 'Hajapata kuabudiwa Mwenyezi Mungu kwa jambo lolote kama Albadaa" (2) katukuka Mwenyezi Mungu na hayo kutukuka kukubwa kabisa.

Tazama ndugu yangu Muislam jinsi wanavyo mnasibishia Allah sifa ya ujinga. Ilihali Mwenyezi Mungu anasema: " Hakuna alioko katika Mbingu na Ardhi ajuae Ghaibu (yasio onekana au hayaja tokea) ila Mwenyezi Mungu" Annaml 65

Badala yake wanaitakidi kuwa Maimamu wao wanajua elimu zote, wala halifichikani kwao jambo lolote. Je hii inaweza kuwa itikadi ya Uislamu aliyo kujanayo Muhammad (s.a.w)?

---

(1) Rejea; Usuullkaafi uk.40

(2) Rejea: Usuululkaafi cha Alkulayny katika kitabu tauhiid (1/331)

*NI IPI ITIKADI YA RAFIDHWA KUHUSU SIFA ZA ALLAH?*

Raafidhwa ndio watu (kundi) wa mwanzo waliopinga sifa za Allah na kudai kuwa kumthibitishia baadhi ya sifa ni kumfanya kuwa ana kiwiliwili. Sheikhul-islamu ibnu taymiya kamtaja mtu wa kwanza kuleta itikadi hii katika Raafidhwa kuwa ni Hisham bin Al-hakam(1) na Hishamu bin Saalim aljawaliiqiy na Yunusi bin Abdirahamani Alqummiy na abuu jaafari al-ahwal(2).

Wote waliotajwa hapo juu ni katika mashekhe wakubwa wa Ithnashariya,kisha wakawa jahmiyya wanaopinga sifa za Allah,kama vile wengi wao katika riwaya zao nyingi walivyomsifu mwenyezi mungu kwa sifa mbaya ambazo waliziambatanisha na sifa ambazo zinathibiti kwa Allah(s.w)

Amepokea Ibnu Baababawaihi zaidi ya riwaya sabini (70) zinazosema kuwa Allah, "hasifiki kwa zama,wala sehemu,wala namna,wala kutikisika, wala kuhama toka sehemu hadi sehemu nyingine,wala hana sifa miongoni mwa sifa za kimaumbile,wala huwezi kumuhisi,wala yeye si kiwiliwili,wala hana sura".(3)

Na kwahiyo mashekhe wao wakafuata njia hii potofu,pamoja na kuzikataa sifa za Allah zilizo thibit katika Qur-an na Sunna za mtume (s.a.w)

Vilevile wanapinga na kukataa kuteremka kwa Allah (s.w)katika mbingu ya dunia katika theluthi ya usiku kama ilivyo thibiti katika hadithi sahihi,na wanasema kwamba Qur-an imeumbwa (sio maneno ya Allah) na wanapinga kumuona Allah siku ya kiyam(hataonekana).

Imekuja katika kitabu (Bihaarul-an-waar) kwamba Abuu Abdillah Jaafar Asaadiq,aliulizwa kuhusu Allah(s.w) je ataonekana siku ya Qiyama?

Akasema ametakasika mwenyezi mungu na hilo kutakasika kuliko kukubwa,hakika macho hayaoni isipokuwa kitu chenye rangi na umbile,na mwenyezimungu ndie muumbaji wa rangi na maumbile(4).

Bali wamesema, lau kama mtu atamnasibisha Allah na baadhi ya sifa, kama vile kuonekana, basi anahukumiwa kama ameritadi (katoka katika uislamu). Haya yamepokewa kutoka kwa shekhe wao Jaafar Annajafy(5).

---

(1)Rejea;Minhaaju sunna(1/20) cha sheikh Ibnu Taymiya.
(2)Rejea Itiqaadaatu firaqulmuslimiin walmushrikina uk.97
(3)Rejea; attauhiid cha Baabawayhi uk 57
(4)Rejea: Bihaarul-answer cha al majlis (4/31)
(5)Rejea: kashful ghitwai ukurasa wa 471

Lakini ni muhimu utambue (ndugu msomaji wa kitabi hiki) kwamba Allah kathibitisha mwenyewe katika Qur-ani kuwa waumini watamuona siku ya qiyama kama ilivyo kuja katika suratl qiyama "*Nyuso sikuhiyo zitakuwa ni zenye kung'ara.ni zenye kumtazama mola wake*."alqiyama:22-23.

Naimethibiti katika sunna sahihi za mtume,kama ilivyo katika sahihi al bukhari na muslim,katika hadithi ya Juraiji bin Abdillah Albajaly, kasema: "Tulikuwa tumeketi na mtume (s.a.w)akautazama mwezi usiku wa tarehe 14 akasema:" "Hakika mtamuona mola wenu kama mnavyouona mwezi huu, hampati shida katika kuuangalia."(1)

Na aya na hadithi zinazothibitisha jambo hili ni nyingi hatuwezi kuziorodhesha zote.

1-Rejea katika bukhari no(544) na muslim no:(633) kwa faida

*NI IPI ITIKADI YA RAAFIDHWA KUHUSU QUR-ANI HII TULIYONAYO AMBAYO ALLAH KACHUKUA AHADI YA KUIHIFADHI?*

Hakika Raafidhwa,ambao katika zama zetu ndio wanaitwa (SHIA) wanasema: Hakika Qur-ani tuliyonayo siyo Qur-ani ile aliyoiteremsha Allah(s.w) kwa mtume (s.a.w) bali imebadilishwa, ikazidishwa na kupunguzwa.

Na jamuhuri wa wanachuoni wa hadithi wa kishia wanaitakidi kwamba Qur-ani imebadilishw, hii ni kwa mujibu wa maneno ya Annuri attwabrisiy katika kitabu chake (Faslul-khitwaab fii tahriif kitabu rabl-arbaab)(1)

Na amesema Mohammad ibn Yaaqub Alkulayny, katika kitabu chake (Usuulul kafi) katika mlango aliouita (Hawakuikusanya Qur-ani yote isipokuwa maimamu)(anakusudia maimamu wao) kisha akaleta riwaya ifuatayo: "Kutoka kwa Jaabir, amesema:nilimsikia Abu Jaafar akisema: Hajapata kudai mtu yoyote kuwa kaikusanya Qur-ani yote kama alivyo iteremsha Allah ispokuwa atakuwa ni muongo. Hakuna alieikusanya na kuihifadhi kama alivyoiteremsha Allah ispokuwa Ally bin Abii Twaalib na maimamu baada yake"(2).

Na imepokewa toka kwa Jaabir toka kwa Jaafar (mwenyezimungu amrehemu) kwamba amesema: "Hawezi kudai mtu yoyote kwamba anayo Qur-ani kamili ispokuwa walioachiwa wasia"(3)

1-Rejea: Faslulkhitwab cha Hussein bin Mahdi Taqiyyun-nuury Ahwabrasy uk.32
2-Rejea: Usululkaafi cha Alkulayn (1/228)
3-Rejea: Usululkafi cha Alkulayn (1/285)

Na imepokewa kutoka kwa Hisham bin Saalim, toka kwa Abii Abdillah (Jaafari) amesema: "Hakika Qur-ani aliyokujanayo Jibrilu kwa mtume (s.a.w) ni aya 17,000."(1)

Maana ya maneno hayo ni kwamba Qur-ani wanayoidai Raafidhwa ni zaidi ua Qur-ani hii tuliyonayo, ambayo Allah kachukua ahadi ya kuihifadhi zaidi ya mara tatu. Tunamuomba Allah atukinge na upotevu wao.

Na ametaja Ahmadi Attwabrisi katika kitabu chake (*Al-ihtiyaaJ*) kwamba Omar alimwambia Zaid bin Thaabit: Hakika Ally alikuja na Qur-ani, ndani mnafedheha za muhajiriina na answari, na tumeonelea tutaje Qur-ani_ nyingine_na tuyaondoe mambo yote ya fedheha za muhajirin na answari, Zaid akakubaliana nae katika hilo.

Kisha akasema: Endapo mtamaliza kuiandika Qur-ani kama jinsi mtakavyo nyinyi, halafu Ally akadhihirisha Qur-ani aliyonayo, je hatakuwa kabatilisha kazi mliyoifanya?. Omar akasema: hivyo ni lipi la kufanya? Zaid akasema: wewe ndio utajua ufumbuzi, Omar akasema: Hakuna ujanja zaidi ya kumuuwa Ally ili tupate kupumua, akafanya mipango ya kumuuwa Ally kupitia Khaalid bin Waliid, lakini hakuweza.

Pindi Omar alipotawala ukhalifa, alimuomba Ally awape Qur-ani ili waibadilishe,akasema Umar: Ewe abal hassan(Ally) Waonaje ungetuletea Qur-ani uliyokuwa umeileta kwa Abuu Bakari ili tuwaunganishe watu katika msahafu mmoja? Akasena (Ally) Hakuna uezekano wa jambo ulitakalo, kwani nilikuwa nimeuleta kwa Abuu Bakari ili kunsimamishia hoja na ili msijekusema siku ya Qiyama "*Hakika sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo*" Surat al aaraaf: 172 au msijekusema "*Haikutujia*" Al araaf: 129, hakika hii Qur-ani hawaigusi isipokuwa walio twaharika, na wale waliousiwa katika wanangu(kizazi changu). Omar akasema: je kunamuda maalumu wa kuidhihirisha? Ally akasema: Ni pale atakapo simama mtoto katika watoto wangu akiidhihirisha na kuwaamrisha watu kuifuata.(2)

---

1-Rejea: usululkaaf cha alkulayny (2/634) kathibitisha shekhe wo riwaya hii katika kitabu chake (Qiraatu al-uquul) (12 525) Akasema: hadithi hii ni thiqa(yakutegemewa)

2-Rejea: Al-ihtijaaj cha Attwabrisy, uk. 225 na kitabu Faslulkhitwab uk. 7

Na kwa vyovyote vile watakavyo jidai Mashia kukikana kitabu (Annur) cha Attwabrisy, Kwa itikadi yao ya (Taqiya), Hakika kitabu hicho kimejaa(kimesheheni) mamia ya dalili toka kwa wanazuoni wao katika vitabu vyao tegemezi, zinazothibitisha kwamba wao wanaitikadi na kuamini kuwa Qur-ani imebadilishwa isipokuwa hawapendi kuamsha makelele ( na malumbano) kuhusu itikadi yao hii juu ya Qur-ani.

Na inabain kuwa kuna Qur-ani mbili, moja inayojulikana kwa waislamu wote, na nyingine ni makhsusi(maalumu) imefichwa, na hiyo ndio kunapatikana ndani yake surat Al wilaya, ambayo mashia wanadai kwamba iliondolewa katika Qur-ani.

Pia katika aya ambazo wanadai kufutwa katika Qur-ani, ni ile aliyoitaja Amry Attwabrasy katika kitabu chake **(***Faslulkhitwab fii tahriif titab rabil arbaab*) ambayo ni (Na tukainua utajo wako kwa ally ambaye ni mkwe wako) Wanadai imeondolewa katika suratl-inshiraah(alam nashrah) wala hawaoni haya katika madai yao haya hali yakuwa wanajua wazi kuwa sura hii ni makkiyyah(imeteremshwa makkah) na Ally hakuwa mkwe wa mtume makkah.

## *NI IPI ITIKADI YA RAAFIDWA KUHUSU MASWAHABA WA MTUME (S.A.W)*

Imejengeka itikadi ya Raafidwa juu ya kuwatukana na kuwakufurisha masahaba wa mtume (s.a.w) rehema na amani zishuke juu yao, Ametaja alkulayn katika kitabu(Furuul-kaafy) kutoka kwa Jaafary (a.s) "waliritadi watu woote baada ya mtume (s.a.w) isipokuwa watu watatu,Nikasema: ni kina nani hao watatu? Akasema ni Miqdaad ibnu As-wad, na Abudhari al-ghifariy, na Salmaan al-faarisy".(1)

Na ametaja Almajlisy katika kitabu (Bihaarul-an-waay) kwamba mtumishi wa Ally ibnul-Husain kasema: Nilikuwa naye (a.s_ katika baadhi ya sehemu alizokuwa akijitenga, nikasema kumwambia: Hakika mimi ninashakia baadhi ya haki kwako,naomba nieleze kuhusu watu hawa wawili, Abubakari na Omar, Akasema: Nimakafiri na kila mwenye kuwapenda ni kafiri". Pia imepokewa toka kwa Abi Hamza Athumaly kwamba alimuuliza Ally bin Alhusain kuhusu Abubakari, Akasema; "Nikafiri na kila atakaemuunga mkono pia ni kafiri.(2)[1]

---

1-Rejea: FURUUL-KAAFY cha Alkulayny uk.115 [1]
2- Rejea:BIHARUL-AN-WAR cha Almajlisy 69/137-138.

Na katika tafsiri ya Alqummy katika kauli yake mwenyezi mungu "Na mwenyezi mungu anakataza kutenda kila makosa, na hasa madhambi yaliyo pita mipaka kwa ubaya, na kila kisicho pendeza, hali kadhalika anakataza kumfanyia ubaya mtu."nnahl ;90" Wametafsiri (Faahisha)Kuw ni Abubakari na (Munkari) Kuwa ni Omar) na (Albagh-yi) Kuwa ni Uthmani.(1)

Na ametaja Almajlisy katika (Biharul-an-war) Kuwa:Habari zinazo onesha(elezea) ukafiri wa Abubakari na Omari na mfano wao, na juu ya malipo ya kuwalaani na kujitenga nao, na habari zinazoelezea uzushi wao ni nyingi kiasi kwamba haitoshi kuelezea katika kitabu hiki au katika vitabu mbalimbali, lakini haya machache tuliyoyataja yanatosha kwa mtu ambae Mwenyezi Mungu kataka kumuongoza katika njia iliyo nyooka.(2)

Bali kataja Almajlis katika (Biharul-an -war) Riwaya mbalimbali kwamba Abubakari na Omar na Uthmani na Muawiya (wenyezi mungu awarehemu) kwamba watakuwa katika masanduku ya moto.(3)

---

Na wanasema(Raafidhwa) katika kitabu chao (Ihqaaql-haq) cha Al-mar-ashy:"Ewe mwenyezi mungu mrehemu muhammad pamoja na ahli zake, na walaani masanamu wawili wa kiquraish, na matwaaghuti wao, na mabinti wao..." (4) wakiwa wanawakusudia Abubakari na Omar na bibi Aisha na Hafswa bint Omar, mwenyezi mungu awarehemu.

1

1-Rejea: Tafsiri ya Alqummy uk 1/390
2-Rejea: Biharul-an-war cha Almajlisy30/230
3-Rejea: Biharul-an-war cha Almajlisy 30/236
4-Rejea: Ihqaaqul-haq 1/337.angalia dua ya masanamu wawili mwisho wa kitabu.

Na ametaja Almajlisy katika risala yake aliyo iita"Al-aqaaid" akasema: Na katika mambo yanayozingatiwa kuwa ni muhimu sana katika dini ya Imaa miyyah ni kuhalalisha Mut-a, na Hajj tamatui, na kujitenga mbali na watu watatu(Abubakari na Omar na Uthumani na Muawiya na Yazid bin Muawiya, na kila aliye mpiga vita Amiril-muuminina Ally) (1)

Na katika siku ya Ashuraa (Rafidhwa)huleta mbwa na wakamita Omar, kisha wanaanza kumpiga kwa fimbo na mawe mpaka anakufa, kisha wanaleta mtoto wa Mbuzi kisha wanamuita Aishan na kisha wanaanza kumnyonyoa manyoya yake na kumpiga hadi anakufa.(2)

Pia huwa wanasherehekea siku aliyo uwawa Omar bin Alkhatwaabi, na wanamuita Abuu luu lu atil-majuusy ambae alimuuwa Omar kuwa ni shuja wa dini(3)

Tunamuomba mwenyezi mungu awarehemu maswahaba wote pamoja wake zake mtume (s.a.w) ambao ni mama w waumini.

Hebu tizama ndigu msomaji ubaya na chuki zilizo bebwa na kundi hili potofu lililo toka katika uislamu, na mambo wanayosema juu ya watu wema kama hawa, ambao ndio watu bora baada ya mitume, watu ambao mwenyezimungu kawasifu, na mtume wake pia, na umma wa kiislamu umekubaliana juu ya uadilifu wao na ubora wao, bali hata historia inashuhudia ubora wao na juhudi zao kubwa katika dini hii ya uislamu.

1-Rejea: Risaalatul-aqaaidi cha Almajlisy uk 85
2-Rejea: Tabdiil dhwalaam wa tanbii haan-myaam cha shekh Ibrahim aljabhaan uk 27
3-Rejea: Abbaasul-qummy (Alkunaa wal-alqaab 2/55

## RAAFIDHWA WANAFANANA NA MAYAHUDI

Amesema sheikhul islamu bin taymiyyah mungu amrehemu,(ushahidi juu ya hilo ni kwamba,Matatizo ya Rafidhwa ndio matatizo ya Mayahudi,Kwa sababu Mayahudi wanasema:Ufalme haupaswi kuwa isipokuwa katika kizazi cha Daudi,Na Raafidwa wanadai kuwa utawala(al imama) haupaswi kuwa isipokuwa kwa mtoto wa Ally (R.A).

Pia mayahudi wanasema:Hakuna jihadi katika njia ya Allah mpaka atakapo kuja Masihi Dajjali ashuke na upanga.Na Raafidwa wanasema: Hakuna jihadi katika njia ya Allah mapaka atakapokuja Mahdi na utoke wito wa jihadi kutoka mbinguni.

Pia Mayahudi hucheleweshа sala zao mpaka nyota zinapo kusanyika, Vilevile Raafidwa nao huchelewesha magharibi mpaka nyota zikusanyike,Ilhali hadithi ya Mtume(S.A.W) Inatufundisha kwamba(*Hautaacha kuwa ummati wangu katika kheri muda wa kuwa hauicheleweshi sala ya magharibi mpaka kukusanyika kwa nyota*)[1]

Mayahudi waliigeuza Taurati,Vilevile Raafidwa nao wameigeuza Qur-ani.

Mayahudi wanapinga jambo la kupangusa katika khofu: Vilevile Raafidhwa wanalipinga jambo hilo.

Mayahudi wanamchukia Malaika Jibrilu, Wanasema: Huyo ni adui yetu miongoni mwa malaika.Vilevile Raafidwa wanasema: Jibrilu alikosea kuleta utume kwa Muhammad(S.A.W).[1]

Vilevile Mayahudi na Wakristo wamewashinda Raafidwa kwa mambo mawili,Kwanza: waliulizwa Mayahudi: Ni nani aliye bora katika watu wa mila yenu? Wakasema: wabora kwetu ni wafuasi wa Musa.Nawa wakristo wakaulizwa:ninani aliebora katika mila yenu? Wakasema: Ni wanafunzi wa nabii Issa(Yesu).

Raafidwa wakaulizwa ninani M-baya zaidi na muovu katika mila yenu? Wakaema wafuasi wa Muhammad(S.A.W)[1]

Na ametaja Sheikh Abdallah al-jamiily katika kitabu chake (Badhlul majhuud fii mushabahati arrafidwa lil yahuud) Kwamba katika mambo mbayo Raafidwa wamefanana na Mayahudi ni,Mayahudi na Maraafidhwa wanawakufurisha watu wote wasiokuwa miongoni mwao na kuzihalalisha damu zao na mali zao,Kisha sheikh akasema: Mayahudi wanawagawa watu katika mafungu mawili tu(Mayahudi na ummamiyuun) Ummamiyuun ni kila asiekuwa Yahudi,na wanaitakidi kwamba wao ndio waumini pekeyao,Ama Ummamiyuun wao ni makafiri

*NI IPI ITIKDI YA RAAFIDWA JUU YA MAIMAMU?*

Raafidwa wanadai maimamu wao ni (Maasuumiin) yaani wamehifadhiwa na madhambi, na kwamba wanajua ghaibu. Kayanukuu haya alkulayniy katika kitabu (usuulul-kaafy) : "Kasema Imamu Jaafar Asswadiq : Sisi ni hazina ya elimu ya Mwenyezimungu, Sisi ni wafasiri wa amri za Mwenyezi Mungu,Sisi ni watu tuliokingwa na dhambi, Imeamrishwa tutiiwe, na imekatazwa tusiasiwe, Sisi ndio hoja ya Mwenyezi Mungu ya wazi kwa viumbe vilivyo chini ya ardhi na mbingu na vilivyo juu ya Ardhi". (1)

Pia kasema Alkulayny katika (Alkaafy) Katika mlango aliouita mlango kuhusu (kwamba maimamu pindi wanapotaka kujua jambo basi hujua tu), Imepokewa toka kwa Jaafar kwamba amesema "Hakika imamu anapotaka kujua basi hujua tu, na kwamba wao wanajua muda wa kufa kuwa ni lini, na kwamba wao hawafi ila kwa hiyari yao wenyewe" (2)

Na amesema Alkhumainiy katika kitabu chake (Tahriirul-wasla) kwamba "Hakika Imamu anayo nafasi tukufu, na daraja ya juu, na utawala wa kufanya kila kitu viko chini ya utawala wake vyote vilivyo katika ulimwengu" na akasema pia "Hakika sisi (anakusudia maimamu wa ithnasharia) tunazo hali Fulani kwa Mwenyei Mungu ambazo hazipati malaika wala nabii yoyote".(3)

(1)Rejea: Usuululkaafy cha Alkulayniy 1/165
(2)Rejea: Usuululkaafy cha Alkulayniy 1/258
(3)Rejea: Tahriirul-walah cha Alkhumainy uk.52,94

---

tu wala hawamjui Allah (s.w).Imekuja katika kitabu chao (Attilmuud) Kwamba: Mataifa yoote wasiokuwa Mayahudi ni washirikina.

Wamemkufurisha hata Nabii Issa (A.S),Kama ilivyokuja katika Attilmuud, wamemsifu na kumtaja kuwa ni kafiri,wala hamjui Mungu.

Raafidwa nao wanaitakidi kwamba wao ndio waumini pekeyao,na kila ambae si Raafidwa basi ni kafiri wala hana fungu lolote katika uislamu.
Ama kuhusu sababu za Raafidwa kuwakakufurisha wailamu ni kwakuwa hawaitakidi(Al wilaya) Ambayo ndio itikadi ya Raafidwa, na kwamba jambo hili ni nguzo katika nguzo za Uislamu na kila asie itakidi hivi basi huyo ni kafiri kwa mujibu wa imani yao ni kama ambae hajatamka shahada mbili,au ni sawa na alie acha sala tano, bali Alwilaya kwao ni jambo ambalo limetangulizwa juu ya nguzo zote za Uislamu.
Amepokea Albarqiyu kutoka kwa Abdallah(a.s) kwamba amesema(hakuna yoyote anaefuata mila ya Ibrahimu isipokuwa sisi tu na wafuasi wetu, Ama watu wengine wote wamejitenga na mila yake.)
Na imekuja katika tafsiri ya Alqummy, kuwa imepokewa kutoka kwa Abdallah(a.s) kwa amesema(Hakuna yoyote alie katika mila ya Uislamu isipokuwa sisi,mpkaka siku ya Qiyama)[1]

Bali imefikia hali kwa Maraafidhwa waliochupa mipaka katika kuwatukuza na kuwafadhilisha (kuwafanya bora) maimamu wao,wamewafanya bora juu ya manabii wote isipokuwa Muhammad (s.a.w) (1)

Hawakuishia hapo tu, bali wanasema kuwa maimamu wao wanautawala wa mwisho kabisa. Ameyataja haya Alkhui katika kitabu chake (Misbaahul-faqaaha) akasema: Ni wazi kwamba hakuna shaka kabisa juu ya utawala wao juu ya viumbe wote, kama ilivyo bainisha katika maneno yao, kwa kuwa wao ndio sababu ya ulimwengu, na wao ndio sababu ya kupatikana viumbe, maana kama si wao basi watu wote wasingeliumbwa, bali wameumbwa kwa ajili yao, na kuwepo kwao ni kwaajili yao….. na utawala walionao maimamu ni kama utawala wa Mwenyezi Mungu juu ya viumbe wake".(2)

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde na upotevu wao huu!! Vipi maimamu wawe ndio sababu ya kupatikana viumbe? Vipi wawe sababu ya kuwepo ulimwengu? Vipi watuwote waumbwe kwaajili ya maimamu wao, ilhali Mwenyezi Mungu anasema katika sura Adhaariyaati 56 "Sikuwaumba majini na watu ila tu wapate kuniabudu".

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atukinge na itikadi potofu kama hii inayopingana na qur-ani na suna za Mtume (s.a.w).

Kasema Sheikhul-islamu bin Tayimiya (Wanadai Raafidwa kuwa dini inafuata matakwa ya wanachuoni wao,halali ni ile wanao ihalalisha wao, na haramu ni ile wanao iharamisha wao,na dini ni yale wanayoyataka wao".

(1) Rejea: mir-aatul-uqual fii shar-hi akhbari rasuul cha Almajlisiy 2/290
(2) Rejea: mis-baulfuqaaha cha Abil-qaasim Alkhui 5/33
(3) Rejea: minhaajusunna cha IbnuTayymiya 1/482.

*NI IPI ITIKADI YA KUREJEA WANAYO IAMINI RAAFIDWA?*

Raafidwa wamezua bid-a (uzushi) wanayoiita (AR-RAJ-A), Kasema Almufiid kuwa: "Wamekubaliana Imamiya juu ya kurudi (kufufuka) wengi katika watu waliokufa".(1)

Na itikadi hii inakusudia kufufuka kwa imamu wao wa mwisho wanaemuita (Al-qaaim) atatoka katika zama za mwisho akitokea katika pango, ambaye atakuja kuwauwa wapinzani wake wote na kuwarejeshea mashie haki zao walizo porwa na makundi mbalimbali katika historia ya kuwepo kwao.(2)

Amesema Assayid almurtadhwa katika kitabu chake (Almasaailu annaaswira) kwamba Abubakari na Omar, watasulubiwa katika zama hizo(za kutoka kwake) huyo imamu wao wa kumi na mbili wanaimuita (Qaaim ahali Muhammad) na kwamba mti utakuwa mbichi kabla ya kusulubiwa kwao lakini baada ya kusulubiwa kwao utakauka.(3)

Na amesema Almajlisy katika kitabu (Haqul-yaqiin) kutoka kwa Muhammad Albaaqir: " pindi atakapodhihiri Almahdi, basi atamfufua bibi Aisha kisha amsimamishie hadd (adhabu)". (4)

Kisha wakayapanua makusudio na maana ya Arraj-a na kudai kuwa Mashia wote watafufuka na maimamu wao, na wagomvi wao nao watafufuka na maimamu wao.

Itikadi hii potofu inatubainishia chuki kubwa zilizo fichika katika nafsi zao ambazo zinawapelekea kueleza upotofu kama huu, na itikadi hii ndio iliwapelekea As-abaiyya wakakanusha kuwepo siku ya mwisho.

(1) Rejea:Awaailul-maqaalaat cha Almufiid uk.5
(2) Rejea:Alkhtuutul-ariidhwa, cha muhibuddin alkhaatwib uk.80
(3) Rejea: Awaailul-maqaalsst cha Almufiid uk.95
(4) Rejea: Haqul-yaqiin cha Muhammadul-baaqir Almajlisy uk.347

Na madhumuni ya kurejea ni kulipiza kisasi kwa wagomvi wao, lakini ni akina nani wagomvi wao? Riwaya ifuatayo itakubainishia ndugu msomaji chuki waliyonayo Raafidhwa dhidi ya Ahlusunna, na jinsi walivyo karibu zaidi na Mayahudi na Manaswara: Ameeleza Almajlisy katika kitabu chake (Biharul-anwar),kutoka kwa Abii baswiir kapokea toka kwa Abu Abdillah(a.w) amesema: alisema: Ewe abu muhmmad: kanakwamba ninatazama kushuka kwa (alqaim) katika masjidis-sahla akiwa na watu wake na familia yake….mpaka akasema… nikamwambia,Atakuwa na msimamo gani kuhusu Ahlu dhimma? Akasema:Atawapa amani kama alivyowapa amani mtume (s.a.w), na watatoa kodi hali ya kuwa ni madhalili,nikasema, je waliokufanyieni uadui? Akasema :Hapa ewe Abu muahammad,yeyote alietukhalifu katika dola yetu hatakuwa na nafasi yoyote, hakika Mwenyezi mungu katuhalalishia damu zao, wakati atakapokuja Alqaim, lakini pindi atakaposimama huyo msimamaji wetu, atalipiza kisasi kwa ajil ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kwaajili yetu pia.91)

Hebu tazama ndugu muislamu jinsi gani huyo Mahdi wa Mashia atawapa amani Mayahudi na Manaswara, halafu awapige vita Ahlu sunna!

(1) Rejea: Biharul-anwar cha Almajlisy 25/376.

*NI IPI ITIKAD YA "TAQIYYAH" KWA RAAFIHDHWA?*

Amesema taqiya mmoja wa wanazuoni wao wa zama hizi kuwa "Taqiya ni kitendo cha mtu kusema au kufanya kinyume na vile anavyo itakidi, kwa lengo la kujikinga na madhara yeye au mali yake au kulinda utu na heshima yake" (1)

Na wanadai kwamba mtume (s.a.w) alifanya (Taqiya) wakati alipokufa kiongozi wa wanafiki Abdallh bin Ubayi bin Saluul, pindi alipokuja kumswalia, kisha Omar (r.a) akamwambia Mtume (s.a.w) Hivi Mwenyezimungu si kakukataza kumsalia mtu huyu mnafiki?, Mtume (s.a.w) akamwambia wewe unajua ni nini nimesema? Nimesema : Ewe mola wangu mjaze ndani yake moto, na ulijaze kaburi lake moto, na umuingize motoni" (2)

Hebu tazama nduguyangu muislamu vipi wanamzulia na kumnasibisha Mtume (s.a.w) na uwongo?! Hivi inaingia akilini kwamba maswahaba wa mtume (s.a.w) wanamtakia reham na Mtume (s.a.w) akimlaani?!.

Na amenukuu Alkulayny katika (Usuulul kafii):"kasema Abu Abdillah : Ewe Omar hakika asilimia tisa ya dini ipo katika taqiya, na hana dini asiyekuwa na Taqiya, na Taqiya inaingia katika kila kitu isipokuwa katika pombe na kupangusa juu ya khofu".

Na amenukuu vilevile Alkulayny toka kwa Abi Abdillah kwamba amesema "icheleeni dini yenu, na ikingeni kwa Taqiya, kwa hakika hana imani asiyekuwa na Taqiya"(3)

---

(1) Rejea: Ashiatul miizaan, cha Muhammad JawadMughniyat uk.47
(2) Rejea: Furuu-ulkafii, kitabul janaiz uk 188
(3) Rejea: Usuulul kafii uk 482-483.

Bali imefikia hali kwa Raafidwa wanajuzisha kuapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa Taqiya!!

Ameyaeleza hayo Alhurul aamily katika kitabu chake (Wasaailu shia) kuwa imepokewa kutoka kwa ibu Bukhari, toka kwa Zuraara toka kwa Abi Jaafar (r.a) amesema: nilisema kumwambia Abu jaafar : Hakika sisi tunapita kwa watu wanatutaka tuape juu ya mali zetu na ilhali tumeshakwisha zitolea zaka, akasema (Abujaafar): Ewe Zurara pindi utakapo chelae hilo basi wewe apa kwa vyovyote vile watakavyotaka,Nikamuuliza : Hata kuapa kwa talaka? Akasema kwa chochote watakacho taka.

Na imepokewa toka kwa Sumaa toka kwa Abii Abdillah (a.s) amesema: "Pindi mtu atakapo apa kwa Taqiya hakuna tatizo maadam kalazimishwa, na kalazimika kufanya hivyo".(1)

Raafidhwa wanaitakidi kuwa Taqiya ni faradhi ambayo madhehebu yao hayasimami bila ya Taqiya, na wanaitumia hasahasa katika mazingira magumu, hivyo inatakiwa ndugu muislamu utahadhari sana na hawa Raafidhwa.

(1) Rejea: wasaailu shia cha Al-hurril-omily 16/136-137.

*NI IPI ITIKADI YA UDONGO WANAYOIAMINI RAAFIDHWA?*

Makusudio ya udongo katika itikadi ya Raafidhwa, ni udongo wa kaburi ya Hussein (r.a) Ameeleza mmoja wa wapotevu miongoni mwao aitwae Muhammad Amnuumanul-haarithy,ambae wanamuita (Asheikhul mufiid) katika kitabu chake (Al mazaar) imepokewa kutoka kwa Abi Abdillah kwamba amesema:" katika udongo wa kaburi ya Hussein,kunapatikana ponyo la kila maradhi,nao ndio dawa iliyo kubwa kabisa'.

Na amesema Abdallah : wafanyieni tahniki ( yaani watilieni mdomoni mara tu baada ya kuzaliwa kwao) watotowenu kwa udongo wa kaburi ya Hussein.

Na akasema vilevile: Alitumiwa Abdul Hussein Arridhwa mzigo (furushi la nguo) kutoka khurasaan ndani yake mkiwa na udongo,akaulizwa alie tumwamzigo huo, Ni kitu gain hiki? Akasema:Huu ni udongo kutoka katika kaburi ya Hussein.Hapakuwa panatumwa mzigo wowote isipokuwa ndaniyake panawekwa udongo, anasema:Udongo huu ni amani kwa idhini ya Mwenyezi mungu. Na inasemakana kwambamtu mmoja alimuuliza swaadiq kuhusu kutumia udongo wa kaburi la Hussein, akajibu kumwambia: Pindi utakapoula basi sema hivi: Ewe Mola wangu hakika mimi nakuomba kwa haki ya ufalme ulioushika,na kwa haki ya Mtume aliye hifahiwa,nakuomba umpe rehma Muhammda (s.a.w) pamoja na watu wa nyumba yake, na ujaalie udongo huu kuwa ni ponyo la kila ugonjwa,na uwe ni kitulizo cha amani kutokana na kila khofu, na niulinzi kutokana na kila baya.

Pia Raafidhwa wanadai kwamba, Mashia wameumbwa kwa udongo maalum,na Sunni wameumbwa kwa udongo mwingine kisha ukachanganywa udongo huo wote,basi maasi na maovu yanayofanya Mshia yeyote ni kutokana na athari ya udongo walioumbiwa Masunni. Na kheri na uongofu anaekuwanayo Sunii yeyote ni kutokana na athari za Udongo walioumbwa shia.Pidni itakapofika siku ya qiyama, basi maovu ya Mashia watabebeshwa Masunni, na mema ya Masunni watapewa Shia.(1)

(1) Rejea: Ilaalu asharaa uk. 490-491. Biharul anwar 5/247-248

*NI IPI ITIKADI YA RAAFIDWA KUHUSU AHLU SUNNAH*?

Miongoni mwa itikadi mbaya za Raafidwa ni kwamba wanahalalisha damu na mali za Ahlu sunnah Amepokea aswadiq katika (Al-ilal) kutoka kwa Daa-uudi bin Farqad amesema: "Nilimuuliza abu abdillah, unasemaje kuhusu Naasiby? (Naswibi wanakusudia Ahlusunnah), akasema:Damu yake ni halali, hatakama utaweza kumuangushia ukuta au kumzamisha baharini basi fanya hivyo.Nikamuuliza vipi kuhusu mali yake? Akasema pindi utakapoweza kuichukua basi ichukue".(1)

Pia Raafidhwa wanaitakidi kwamba kizazichao ndio kizazi safi, Ameeleza Hashimu Albaharany katika tafsiri yake(Alburhan) imepokewa toka kwa maytham bin Yahya,kutoka kwa Jaabir bin Muhammad, amesema"Hakuna mtoto yoyote azaliwaye isipokuwa Ibilisi anakuwa haadhir katika kuzaliwa kwake,anapojua mtotohuyo ni katika Shia basi shetani mkubwa anamkinga huyo mtoto kutokanan na ibilisi, na kama sio katika shia basi shetani huingiza kidolechake katika sehemu zake za nyuma(katika makalio ya mtoto), nah ii ndio sababu ya kuwa mtoto wa kiume huzaliwa kaelekea chini, na kama ni mtoto wa kike basi shetani huingiza kidole chake katika utupu wake, hivyo anazaliwa akiwa ni muovu, na ndio maana mtoto huzaliwa analia sana"(2)

Bali mashie wanaitakidi kwamba watu wote ni watoto wa zinaa isipokuwa Shia peke yao!! Ameeleza Alkulayny katika kitabu chake (Arraudhwatu minalkafi) kutoka kwa Abi Hamza,kutoka kwa Abu Jaafar (a.s) kwamba amesema: "Nilisema kumwambia, hakika baadhi ya jamaa zetu wanazua uwongo na kuwatuhumu wasio waungu mkono, akamjibu kuwa, kuachana nao ni bora zaidi, kasha akasenma: Wallah ewe Abu Hamza hakika watu wote ni watoto wa zinaa isipokuwa Shia".(3)

---

(1) Rejea: almahaasin Annafsaaniya uk166
(2)Rejea: Tafsirul burhani cha Hashim Albahrany 2/300
(3) Rejea: Arraudhwatul minalkafi cha Alkulayny 8/285.

Na katika itikadi za raafidwa wanaona kwamba Ahlusunna ukafiri wao ni mkubwa zaidi kuliko ukafiri wa Mayahudi na manaswara, kwa sababu wao asili yao ni Makafiri, ama Ahlisunna kwamba wao wameritadi,na ukafiri wa kuritadi ni mkubwa zaidi, hii ni kwa mujibu wa ijmai, na ndio mana wanakuwa bega kwa bega dhidi ya waislamu, kama historia inavyojieleza.(3)

Imekuja katika kitabu (wasaailu shia) kutoka kwa Alfudhwail bin yasaar amesema: "Nilimuuliza Abu Jaafar je naruhusiwa kumuozesha Naswibii mwanamke wa kirafidwa? Akasema: Hapana, kwa sababu Naswibii ni kafiri" (4)

Na manaswibii kwa ahlusunna ni wale ambao wanamchukia Ally bin Abitwaalib(r.a), lakini Raafidwa wao wanawaita ahlusunna Naswibii, kwa sababu wanamtanguliza Abubakari na Omar na Uthmani juu yaAlly, pamoja na kwamba kumtanguliza Abubakari na Omar n Uthmani juu ya Ally ndivyo ilivyo kuwa zama za Mtume (s.a.w), na ushahidi wa haya ni kauli ya ibni Omar: ". Na amezidisha Attwabrani katika Alkabiir: "Tulikuwa tukifadhilishwa baina ya watu katika zama za (s.a.w) tunamfadhilisha Abubakari kisha Omar Kisha Uthmani " Amepokea bukhari. Na amezidisha Attwabrani katika alkabiir: "Na Mtume (s.a.w) alikuwa akilijua hilo wala hatukemei katika hilo". Pia ibnu Asskir amesema :"tulikuwa tukimfadhilisha Abubakari na Omar na Uthmani na Ally".

Amepokea imamu Ahmad na wengineo kutoka kwa Ally bin Abi twalib kwamba amesema: Mbora wa umma huu baada ya Mtume (s.a.w) ni Abubakari kisha Omar, na laiti ningependa ningemtaja wa tatu". Amesema Imamu Ahnad kwamba athari hii ni mutawaatir.(5)

(4) Rejea: wasaail shia cha Alhurul aamily (7/431) Attahdhiib (7303)
(5)Attaaliqaat alaa matni lumuatul-iitqaad cha sheikh Jibrin uk.910

## *NI IPI ITIKADI YA RAAFIDHWA KUHUSU NDOA YA MUT'A NA INA UBORA GANI KWAO?*

Ndoa ya mut'a inafadhila kubwa kwa Raafidhwa, kama wanavyo dai, imekuja katika kitabu (Manhaju sswadiqiin) cha fat'hullah Alkaashan, kapoke a toka kwa Asswaadiq: Hakika Mut'a ni katika dini yangu na dini ya baba yangu, basi mwenye kuifanya hiyo anatekeleza dini yetu, na mwenye kuipinga,huyo atakuwa anaipinga dini yetu, bali huyo anaifuata dini nyingine isiyokuwa dini yetu, Na mtoto anaezaliwa katika ndo ya mut'a ni bora kuliko anaezaliwa katika ndoa ya kawaida, Na mwenye kuipinga mut'a huyo ni kafiri ameritadi, (1)

Amenukuu Alqummy katika kitabu (Man laa yahdhuruhul- faqiih) kutoka kwa abdallah bin sinani, kutoka kwa Abdillah amesema: "Hakika mwenyezi mungu mtukufu katuharamishia kinyaji chochote chenye kulevya, na akatupa badalayake mut'a" (2)

Naimekuja katika (Tafsiri ya manhaju sswaadiqiin) ya Mullah Fat'hullah Alkaashaany: "Amesema mtume (s.a.w) Mwenye kufanya mut'a mara moja, basi huachwa huru na moto theluthi yake, na mwenye kufanya mara mbili huachwa huru na moto theluthi mbili, na mwenye kufanya mara tatu,basi huachwa huru na moto yeye mzima"

Na katika kitabu hichohicho, imekuja kuwa "kasema Mtume (s.a.w) mwenye kufanya mut'a mara moja, basi huyo kasalimika na ghadhabu za Mwenyezi mungu, na atakae fanya mara mbili atafufuliwa pamoja na watu wema, na atakaefanya mara tatu huyo atakuwa nami peponi".

Pia katika kitabu hichohicho kwamba amesema Mtume(s.a.w) mwenye kufanya mut'a mara moja, anakuwa katika daraja ya Hussein, na mwenye kufanya mut'a mara mbili yuko katika daraja ya Hassan, na mwenye kufanya mut'a mara tatu, anakuwa katika daraja ya ally bin Abitwaalib, na mwenye kufanya mara nne daraja yake ni kama daraja yangu"(3)

(1) Rejea: manhaju sswaadiqiin cha Mullah Fut'hullah Alkaashany 2/495
(2) Rejea;man laa yah dhuruhulfaqiih cha ibnu baabawaihi Alqummy uk. 330
(3) Rejea: Tafsir Manhaju sswaadiqiin cha mullah Fut'hullah Alkaashany 2/ 492-493

Na marafidhwa hawakuainisha idadi maalumu katika swala la mut'a, imekuja katika (Furuu ul kaafy) na (Attahdhib) na (al-istibuswari) kutoka kwa Zuraara kapokeya toka kwa Abiabdillah, kasema :"Aliulizwa kuhusu mut'a kwamba je nikatika wanawake wa nne walio ruhusiwa? Akasema:waweza kuowa mpaka elfu moja, kwa sababu wao ni mwenye kukodiwa. Na pia imepokewa kutoka kwa Muhammad bin muslim, kutoka kwa Abi Jaafar kwamba, alisema kuhusu ndoa ya mut'a: kwamba hao sikatika wale wa nne, kwa sababu mwanamke anaye olewa ndoa ya mut'a hapewi talaka, wala hana fungu lolote katika mirathi,bali yeye ni mwenye kukodiwa tu ".(1)

Vipi hali hii na ilihali Mwenyezi Mungu anasema "Na wale ambao tupu zao wanazilinda.Isipokua kwa wake zao au kwa (wanamwake) wale iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, basi hao ndio wasio laumiwa.(Lakini)Anaye taka kinyume cha haya basi hao ndio warukao mipaka (Ya Mwenyezi Mungu).(Almu-uminun 5-7).

Kwa hiyo aya hizi zinatubainishia kwamba ndoa zinazo ruhusiwa ni mke na wale iliyo wamiliki mikono ya kuume,na kinyume na hawa basi ni haramu, hivyo mut'a ni zinaa, tunamuomba Mwenyezi Mungu atukinge na shari.

Amesema sheihk Abdallah bin Jibrin kwamba (Raafidhwa katika kuhalalisha mut'a wanaitumia aya iliyokuja katika suratun nisaai aya ya 24 " *Na pia (mmeharamishiwa)wanawake wenye(waume zao) isipokua wale iliyo wamiliki mikono yenu ya kuume(ndio)sheriya ya Mwenyezi Mungu juu yenu.Na mmehalalishiwa(kuowa wanawake)wasio hawa muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaowa bila ya kufanya zinaa. Basi wale mnao waowa miongoni mwao wapeni mahari yao yalyio lazimishwa .Wala si vibaya kwenu katika (kutoa) yale mliyo ridhiana badala ya yale yaliyo tajwa.Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi na mwenye hekima*."Annisaai:24

(1) Rejea: Alfuruu minal kaafi cha Alkulayny 5/451 na Attahdhib 2/188.

Na jawabu la hoja hii ni kwamba: Hakika aya zote hizi kuanzia aya ya 19 hadi aya ya 23 zinazungumzia ndoa, kisha baada ya kutaja wale walio haramishwa kwa nasabu na kwa sababu zingine akasema Mwenyezi Mungu "*Mmehalalishiwa wanawake wengine wasio kuwa hawa walio tajwa, basi pindi mtakapo waoa ili kustarehe nao kihalali, basi wapeni mahari zao mlizo kubaliana, na kama wakisamehe chochote katika hizo mahari zao kwa ridhaa zao basi hakuna ubaya katika hilo."* hivyo ndivyo walivyo ifasiri aya hii kongamano la maswahaba na walio kuja baada yao".(1)

Hata Shekh wa kundi la Attusy katika kitabu chake (Tahadhiibul-ahkaam)ameitaja kwa ubaya ndoa ya Mut`a, anasema:"Kama akiwa mwanamke anatoka katika nyumba ya watu watukufu basi haifai kumuoa katika ndoa ya mut`a, kwa kuchelea aibu itakayo ipata familia yake na udhahalili utakao mpata yeye". (2)

Bali hali imefikia kwa hawa Rafidhwa wanahalalisha kumuendea mwanamke kinyume cha maumbile.Yamekuja haya katika (Al-istibswaar)kutoka kwa Ally bin Alhakam amesema;"Nilimsikia swaf wani anasema:Nilimuuliza Ar-ridhwaa nikasema:Hakika mmoja katika wafuasi wako kanituma nikuulize jambo ambalo yeye kaogopa na kaona aibu kukuuliza,akasema;nilipi ?akasema:Je inafaa mtu kumuingili mke wake kinyume cha maumbile? Akasema:Ndio inafaa." (3)

---

(1) Ni katika maneno ya Shekhe Ibnu Jibrin.na dalili nyingine ya kuharamisha mut`a katika suna za Mtume(s.a.w) ni Hadithi ya Rabiu bin Sabura Aljuhany kwamba babayake alimuhadithia kwamba alikuwa pamoja na Mtume (s.a.w) akasema:"Enyi watu hakika mimi nilkuwa nimekuruhusuni kufanya Mut`a ,hakika Mwenyezi mungu ameiharamisha mpaka siku ya Qiyama,yoyote ataye kuwa na mwanamke ambaye kamuoa ndoa ya Mut`a basi na amuache,na wala asichukue chochote alichokuwa kampa". Kaipoke Muslim Nnambari (1406).

(2)Rejea: Tahdhiibul-ahkaam cha attusy 7/227 .

(3) Rejea: Al-istibswaar cha Attuusy (3/243).

## *NI IPI ITIKADI YA RAFIDHWA KUHUSU NAJAF NA KAR-BALAA,NA JE KUNA FADHILA GANI KATIKA KUZURU SEHEMU HIZI?*

Mashia wanaitakidi sehemu yalipo makaburi ya watu walio dai kuwa ni maimamu wao, au ambao ni maimamu kweli, kwa sehemu hizo ni sehemu takatifu,hivyo Alkuufa ni haram(sehemu takatifu),pia Kar-balaa ni haram,na Qumm nayo ni haram. Na wanayo riwaya wanayo dai kuwa imepokelewa kwa Asswaadiq kwamba, Mwenyezi mungu anayo haram yake ambayo ni makka,na Mtume wake anayo haram yake ambayo ni Madina,na amiiril-mu`uminiina anayo haram yake ambayo ni Alkuufa,na sisi tunayo haram yetu ambayo ni qumm.

Na Kar-balaa kwa Mashia ni bora kulikko Alqaaba. Imekuja katika kitabu(Bihaarul-anwar)kutoka kwa Abii Abdillah kwamba kasema; "Hakika Mwenyezi mungu aliiteremshia Alqaaba wahyi(ufunuo)lau kama si udongo wa Kar-balaa nisingelikufanya bora ,na lau kama si mwili wa yule aliyeko katika udongo wa Kar-balaa nisingekuumba,wala nisinge umba nyuba ambayo kwayo umejifakharisha,basi tulia na uwe ni Mkia dhalili na si mwenye kibri kwa ardhi ya kar-balaa,la sivyo nitakutupa katika Jahannam" (1)

Bali rafidhwa wanaona kuzuru kaburi la Husein huko karbalaa ni bora kuliko nguzo ya tano ya uislamu(Hijja)!!. Amesema Almajlisy katika kitabu chake (Bihaarul-anwar)Kutoka kwa bashiir addahaan amesema;"Nilimuuliza Abuu Abdillah(a.s) Endapo itanipita hijja alafu nikaenda katika kaburi ya Husein? Akasema:Vizuri sana ewe Bashir,muumini yeyote atakae liendea kaburi la Husein hali ya kutambua haki yake,katika siku ambayo sio siku ya idd,basi huandikiwa thawabu za Hijja 20 na Umra20 zenye kukubaliwa,na thawabu za kushiriki katika vita 20 vya Jihadi pamoja na Mtume au Imamu muadilifu, na atakaye liendea siku ya Arafa hali ya kujua haki zake basi huandikiwa thawabu za Hijja 1000 na Umra 1000 zenye kukubaliwa,na thawabu za kupigana Jihadi 1000 pamoja na Mtume au Imamu muadilifu.

---

(1)Rejea kitabu Albihaar(10/107)

Pia katika kitabu hicho hicho wametaja kwamba wanao zuru kaburi la hussein huko karbalaa ni watu safi,na wanaokuwa wamesimama Arafa ni watoto wa Zinaa!!"imepokewa toka kwa Ally bin Asbaatwi kwamba kapokea toka kwa Abi Abdillah(a.s) kuwa kasema:Hakika Mwenyezi mungu Mtukufu anaanza kuwatazama wanao zuru kaburi la hussein usiku wa kuamkia Arafa.Akasema:Nikamuuliza,Kabla hajawatazama walioko katika kisimamo cha Arafa?akasema;Ndio,nikamuuliza,kwanini iwe hivyo? akasema: Kwa sababu katika watu walioko Arafa mna watoto wa zinaa tofauti na wale walioko Karbalaa hakuna mtoto wa zinaa kati yao". (1)

Bali kiongozi wao mkuu Ally Assistaany katika kitabu chake(Minhaajus-swaalihina)Amefadhilisha kuswali katika makaburi kuliko kuswali katika Miskiti!! Kasema katika mas-ala nambari 562:Inapendeza kuswali katika makaburi ya maimamu (a.s)bali imesemekana kuwa ni bora kuliko kuswali miskitini, na imepokewa kwamba kuswali katika kaburi la imamau ally bin Abi twaalib(a.s)ina ubora wa swala laki mbili. (2)

Bali Shekh wao Abbas Alkaashaany katika kitabuchake(Maswaabiihul-jinaani)kapituka mipaka katika kuitukuza Karbalaa mpaka akasema:" Hapana shaka kwamba Karbalaa ndio sehemu takatifu zaidi katika uislamu,na imepewa utukufu ambao haikupewa sehemu yoyote ardhini,na hii ni kwa mujibu wa dalili nyingi zilizo pokewa kuhusu jambo hili,hivyo ikafanywa ndio ardhi ya Allah(s.w)iliyo tukuzwa na kubarikiwa,na ni ardhi iliyo nyenyekea, na ni ardhi iliyo teuliwa na ndio haram ya Alla yenye baraka na amani,na ndio haram ya Mtume,na ndio kitovu cha uislamu,na ni katika sehemu ambazo Allah anapenda kuomba na kuabudiwa katika sehemu hizo,na ndio ardhi ambayo udongo wake ni tiba, hakika sifa hizi na nyinginezo zilizopo katika ardhi ya karbalaa,hazipatikani katika sehemu yoyote ardhini,hata katika alkaaba". (3)

---

(1) Rejea;Bihaarul-anwar cha Almajsliy 85/98
(2) Rejea:Minhaajus-swalihiin cha Assisaany 1/187
(3)Rejea; Maswaabiihul-jinaan cha Abbaasi Alkaashaany uk 360.

Pia imekuja katika kitabu(Almazaar) cha Muhammad Annuumaan,wenyewe wanamuita (Ashaikhulmufiid) akielezea ubora wa Masjid alkuufa:Imepokewa toka kwa Abii Jaafar Albaaqir amesema:"Lau watu wangejua fadhila zinazo patikana katika masjidulkuufa basi wangeliuandalia matumizi na vipandwa kutoka sehemu mbalimbli ili kuuendea,hakika swala ya faradhi katika msikiti huo ni sawa na Hijja ,na swala ya sunna ni sawa na umra."(1)

Pia imekuja katika kitabu hicho hicho katika mlango aliyo uita (Yasemwayo wakati wa kusimama katika kaburi) kwamba mwenye kumzuru Hussein anatakiwa kuashiria kwa mkono wake wa kuume, na aseme katika dua ndefu kabisa,miongoni mwake maneno yafuatayo:"Nimekujia kukuzuru,nikitaraji uthibitishwe unyayo wangu,na nina yaqini kwamba Mwenyezi mungu Mtukufu anawaondolea waja wake matatizo yao kupitia kwenu, na kwa sababu yenu anateremsha rehma,na kupitia nyinyi anaizuia ardhi isiwadidimize watu wake,na kupitia nyinyi kayathibitisha mjabali yake.Ninamuelekea Mola wangu kupitia kwenu ili mnikidhie haja zangu,na mnisamehe madhambi yangu."(2)

Hebu tazama ndugu msomaji jinsi watu hawa walivyo tumbukia katika ushirikina ,kwa kumuomba asiye kuwa Allah awakidhie haja zao,na kuomba kusamehewa madhambi yao kwa asiye kuwa Allah, vipi wamefikia katika hali hii,na ilihali Mwenyezi Mungu anasema"Hakuna anaye samehe madhambi ila Allah".Al-imraan: 135. Tunamuomba Allah atukinge na ushirikina.

(1)Rejea:Kitaabul-mazaar cha sheikh Almufiid uk. 20.
(2)Rejea:kitaabul-mazaar cha sheikh Almufiid uk. 99.

## *NI MAMBO GANI AMBAYO RAAFIDHWA WAMETOFAUTIANA NA AHLU SUNNAH?*

Amesema Nidhwaamud-diin muhammad al-a`adhwamy katika utangulizi wa kitabu chake (Ash-shiiatu wal-mut`a) :"Hakika tofauti zilizopo kati yetu na Ahlusunnah sio tofauti za kifiqhi peke yake, kama vile mas`ala ya Mut`a n.k hapana,bali asili ya tofauti zetu ni katika mambo ambayo ndiyo misingi ya dini(Mambo ya kiitikadi) kama haya yafuatayo:

(1) Rafidhwa wanadai kwamba Qur-ani imebadilishwa,hivyo ina mapungufu. Nasisi tunasema:hakika Qur-ani ni maneno ya Allah yaliyo timia wala hayana mapungufu yoyote,hayakubadilishwa,wala hayatabadilishwa aidha kwa kupunguzwa au kuongezwa mpaka siku ya Qiyama. Kama alivyo sema Allah "Hakika sisi tumeuteremsha ukumbusho(Qur-ani),na hakika sisi tutauhifadhi". Alhijri 9

(2) Rafidhwa wanadai kuwa maswahaba wa Mtume(s.a.w) waliritadi baada ya kufa Mtume(s.a.w)ispokuwa wachache tu,na wakafanya khiyana katika dini hasa hasa Makhalifa watatu;Abubakari,Omar na Othman. Na kwa hiyo Makhalifa hawa watatu ni Makafiri na ni wapotevu kwa mujibu wa imani ya kishia. Nasisi tunasema;Hakika maswahaba wa Mtume(s.a.w) ndio viumbe bora baada ya Mitume,na kwamba wote ni waadilifu,hawawezi kumsingizia Mtume(s.a.w),na ni wakweli katika yale waliyo yanukuu kutoka kwa Mtume(s.a.w).

(3) Rafidhwa wanadai kuwa:Hakika maimamu wao kumi na mbili ni maasuumiin(wamehifadhiwa na madhambi),na kwamba wanajua ghaibu na wanayo elimu yote waliyo pewa Malaika ,Manabii na Mitume,na kwamba wanajua mambo yote yaliyo pita na yajayo,halifichikani kwao jambo lolote,na kwamba wao wanazijua lugha zote za ulimwenguni na kwamba dunia yote ni ya kwao. Na sisi tunasema kwamba: Wao ni viumbe kama viumbe wengine,wamo miongoni mwao wanachuoni,na Makhalifa.Wala haifai kuwanasibisha na jambo ambalo wao hawakujinasibisha nalo bali wao walikataza mambo hayo na kujitenga mbali nayo kabisa. (1)

(1)Rejea:Utangulizi wa Nidhwaamud-diin Muhammad Al-aadhwami katika kitabu(Ashiatu wal-Mut`a) uk 6 .

*NI IPI ITIKADI YA RAAFIDWA KUHUSU SIKU YA ASHURAA? NA INAUBORA GANI KWAO?*

Hakika Raafidwa wanafanya mahafali na kuandamana mabarabarani na katika viwanja mbalimbali na kuomboleza na kuvaa mavazi meusi ili kuonyesha huzuni katika kukumbuka kifo cha Hussein (r.a) katika kumi la mwanzo la mwezi wa Muharram kila mwaka.

Wanafanya haya wakiitakidi kuwa jambo hili ni katika njia za kujikurubisha kwa Allah (s.w), wanapiga mashavu yao na vifua vyao na migongo yao na kurarua nguo zao huku wakilia kwa makelele wakisema: Yaa Hussein..Yaa Hussein, Bali hufikia wakajipiga kwa Minyororo na Visu kama ilivyo katika nchi ambazo Raafidhwa ni wengi, kama Irani.

Na masheikh wao wanawahimiza sana katika mambo haya ambayo ni vichekesho kwa mtu mwenye akili timamau kuambiwa kwamba hii ni dini. Aliulizwa mmoja wa masheikh wao mwenye kutegemewa Muhammad Hassan Aalkaashiful-ghitwaa kuhusu mambo wanayoyafanya watu wake? Akasema: Hakika kufanya hivyo ni kuyaadhimisha matukufu ya Mwenyezi Mungu kama ilivyokuja katika Suuratul-Hajj " Mwenye kuheshimu alama za (dini ya) Mwenyezi Mungu, basi hilo ni jambo la ucha Mungu wa nyoyo). Al-hajj 32*

*Mambo haya ya kipuuzi wanayafanya kila mwaka. Na Mtume (s.a.w) amekataza kujipiga mashavu na kuchana nguo… kwa huzuni ya kufiwa, kama ilivyokuja katika Hadithi sahihi iliyopo katika sahihi Muslim Hadithi nambari 103. Lakini Raafidhwa wao huzipiga ukutani hadithi za Mtume (s.a.w) kwa sababu wao ni miongoni mwa makundi yanayo mkadhibisha Mtume (s.a.w).

*NI IPI ITIKADI YA RAAFIDHWA KUHUSU BAY'A (KUTOA AHADI YA KUMTII KIONGOZI).*

Raafidwa wanaitakidi kwamba kila utawala ambao si utawala wa Ithna Ashariya ni batili na haufai. Imekuja katika kitabu (Alkaafiii bisharhil-maazindraany) na katika (Alghaiba) cha Annu-umaany kutoka kwa Abii Jafar amesema:"kila Bendera itakayo inuliwa kabla ya Bendera ya Mahd-wa kiraafidhwa-basi mwenye kunyanyua bendera hiyo ni Twaaghuut".(1)

Wala haifai kumtii mtawala ambae hakuteuliwa na Allah ispokuwa kwa misingi ya Taqiyya, na kiongozi ambae ni jeuri na dhwaalimu ambae hastahiki utawala haifai kumtii; wanawakusudia kwa sifa hizi watawala wote wa kiislamu wasio kuwa katika Maimamu wao, na wamwanzo kabisa katika watawala hao, ni Makhalifa wa Mtume (s.a.w) Abubakari, Omar, na Othman -radhi za Mwenyezi Mungu ziwafikie.

Amesema mmoja katika Raafidwa Almajlisy ambae ni mmoja katika wapotevu wao kasema katika kitabu chake (Bihaarul-anwar) kuhusu Makhalifa hawa watatu: "Hawakuwa ila ni waporaji tu, na niwatawala jeuri, walio ritadi kutoka katika Dini, Mungu awalaani na kila mwenye kuwafuata na kuwaunga mkono katika dhulma yao kwa Ahlul-bait" (2)

Haya ndio maneno ya kiongozi wao Almajlisy ambaye kitabu chake ndio kitabu mama (chenye kutegemewa) katika Hadithi, haya ndio maneno yake kwa watu ambao ndio watu bora baada ya Mitume.

Na kutokana na mtazamo wao huu juu ya Makhalifa wa waislamu basi wamemzingatia kila mwenye kuwakubali ni twaghuti na ni kiongozi jeuri. Amepokea Alkulayny kutoka kwa Omar bin Handhwala kuwa amesema: "Nilimuuliza Abuu Abdillah kwamba ikiwa watu wawili miongoni mwetu watakhtilafiana katika deni au Mirathi kasha wakapelekana kwa Qaadhi au Hakimu jee inafaa? Akasema: atakaetaka kuhukumiwa kwao katika misingi ya haki au baatwili, basi ajue anachukua haram hata kama ni haki yake, kwa sababu atakuwa kaichukua kwa hukumu ya Hakimu ambae ni Twaghuti". (3)

---

(1) Rejea: Alkaafii sherhe ya almazindrany (12/371).Pia tazama Albiharu (25/113)
(2) Rejea: Albihaaru cha Almajlisy (4/385)
(3) Rejea: Alkaafii cha Alkulayny (1/67), (Attahdhiib 6/301), Man laa yahddhurhul-faqiih (3/5).

Amesema Alkhumayny katika kitabu chake (Alhukumatul-Islaamiyya) katika kuelezea mazungumzo yaliyotangulia hapo nyuma "Kiongozi mwenyewe anakataza watu kumuendea Qaadhwi, na analiona jambo hili ni kuwaendea Matwadhuti". (1)

Na imekuja katika kitabu (Attaqiyyatu fii fiqhi Ahlil-bayt) katika mlango wa tisa alipo zungumzia Taqiyya katika Jihadi, na maelezo yake haya ilikuwa ni kuunga Mkono tafiti zilizo fanywa na Mufti wao Ayattullah Alhajji Muslim Addaa-awary alipokuwa akielezea masharti ya kufanya kazi chini ya (mtawala) Dhwaalim- wanakusudia Mtawala yeyote ambae ni katika Ahlusunna-akasema: " Hakika kufanya kazi chini ya Mtawala kumegawanyika sehemu tatu: (a). Kunawakati inakuwa ni kwa nia ya kuwasaidia waumini wenzio.(2) na kusimamia maslahi yao, na kukidhi haja zao, kuingia kwa nia hii hukumu yake ni mustahabu (inapendeza) na imehimizwa kufanya hivyo, (b)Na mara nyingine inakuwa kwa nia ya kutafuta maisha na kujineemesha, kuingia kwa nia hii hukumu yake inajuzu japokuwa ni makuruhu (haiimizwi mtu afanye hivyo) na endapo atawafanyia ihsani ndugu zake waumini na kukidhi haja zao hiyo itakuwa ni kafara kwake, kwa mijibu wa riwaya zilizo kuja zikishartisha hivyo. (c) Na kuna wakati inakuwa ni kwadharura na haja ya kupata riziki (kula na kunywa) hukumu yake inakuwa ni halali na inajuzu bila chukizo lolote" (3)

Hebu tazama ndugu yangu Muislamu jinsi wanavyo wahukumu Ahlu sunna kuwa ni Madhwaalim na waovu!! Na walivyo juzisha kufanya kazi na watawala wa kisunni kwa masharti,. Ambayo miongoni mwayo ni kuwanufaisha Mashia, na hili liko wazi kabisa, maana huwezi kumkuta Shia katika nafasi Fulani ispokuiwa atajitahidi kadri awezavyo amuweke Shia mwenzake na kumuweka mbali kabisa Sunni. Tunamuomba Allah awakinge Waislamu kutokana na shari zao.

(1) Rejea:Alhukuumatul-islamiyya uk.74
(2) Wanaposema waumini wanakusudia (Shia) kwa sababu Raafidhwa wanajiita Waumini.
(3) Rejea: Kitaabu Attaqiyya fii fiqhi Ahlil-bayti cha Sheikh Muslim Addaa-wary (2/153)

*NI IPI HUKUMU YA KUJENGA MAHUSIANO NA UKARIBU KATI YA AHLU SUNNA NA RAAFIDHWA WASHIRIKIN?*

Nitatosheka ndugu msomaji na kutaja makala moja tu miongoni mwa makala za Dr. Naaswir Alqifaary katika kitabu chake ( Mas-alatu taqriib) nayo ni makala ya saba, amesema-Allah amuhifadhi- "Inawezekanaje kujenga mahusiano na ukaribu na watu ambao wanakitoa kasoro kitabu cha Allah na kukifasiri kwa tafsiri zisizo sahihi, na wanadai kuwa Maimamu wao wameteremshiwa Vitabu baada ya Qur-ani (1), Na wanaona kuwa Al imama ni Utume, na Maimamu wao ni kama Manabii au ni wabora kuliko Manabii, na wanaifasiri ibada ya Allah (s.w) pekeyake ambao ndio ujumbe waliokujanao Mitume wote,kwa tafsiri zingine wazijuazo wao tu.

Na wanadai kwamba Ibada ni kuwatii Maimamu, na kwamba Shirki ni kuchanganya Twaa ya Maimamu pamoja na wengine, na wanawakufurisha Maswahaba watukufu wa Mtume (s.a.w) na wanawahukumu Maswahaba wote kwamba waliritadi ispokuwa watatu au wane au saba, kwa mujibu wa Riwaya zao tofautitofauti, na wanatofautiana na Waislamu wote kiitikadi mbalimbali kama vile, itkadi ya Al imama, Al-isma, Attaqiyya n.k na wanaitikadi ya kufufuka Maimamu wao na Mashia wote….." (2)

(1) Tazama ndugu msomaji mwisho wa kitabu hiki moja kati ya Sura ambazo Raafidwa wanadai kwamba zimeondolewa katika Qur-ani ambayo ni Suuratu (Alwilaya) iliyo nukuliwa katika kitabu (Faslul-khitwaab) cha Annuuriy Attwabraasy, nahuku ni kumkadhibisha Allah (s.w) ambae ka ahidi kukihifadhi kitabuchake, aliposema "Hakika sisi tumeuteremsha ukumbusho (Qur-ani) na hakika sisi tutauhifadhi" Alhijr 9. Hivi mtu mwenye akili timamu anaweza kutia shaka juu ya ukafiri wa mwenye kuitakidi itikadi kama hizi?

(2) Rejea: Mas-alatu taqriib cha Sheikh Dr. Naaswir Alqifaary (2/302)

*NI ZIPI NUKUU ZA SALAF NA KHALAF KUHUSU RAAFIDWA?*

Amesema Sheikhl-islaam bin Taymiyya-Allah amrehemu-:"Wamekubaliana wana chuoni kwamba Raafidhwa ni kundi lenye kusema uwongo, na uwongo wao ni watangu".

Amesema Ash-habu bin Abdul azizi: "Aliulizwa Maalik-Mwenyezi Mungu amrehemu- kuhusu Raafidhwa, akasema: usiseme nao, wala usipokee kwao, kwa sababu ni waongo.Na amesema Imamu Maalik: yeyote mwenye kuwatukana Maswahaba wa Mtume (s.a.w) hana jina, au alisema hana fungu lolote katika uislamu".

Na amesema Ibnu Kathiir katika kauli yake Allah (s.w) "Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja nae ni wenye nyoyo thabiti mbele ya Makafiri, na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (Pamoja), Wakitafuta fadhila za Allah na Radhi (zake). Alama zao ziko katika nyuso zao kwa taathira (athari) Ya Kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurat. Na mfano wao katika Injili (umetajwa hivi): kuwa (wao) Ni kama Mmea uliotoa Matawi yake, kisha (Matawi hayo) Yakautia nguvu, ukwa mnene, ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake ukawafurahisha walio upanda".Alfat-hu :29

Akasema "kutokana na riwaya hii Imamu Maalik -Mwenyezi Mungu amrehemu-katoa hukumu ya kuwa Raafidwa kuwa ni Makafiri, wale wanao wakufurisha Maswahaba, akasema: kwa sababu wanawachukia Maswahaba, na mwenye kuwachukia ni kafiri kwa mujibu wa aya hi".

Amesema Qurtuby: " Kwa hakika kafanya vizuri Imamu Maalik katika makala yake haya na katika tafsiri yake hiyo yeyote atakae mdharau mmoja katika Maswahaba, au akamtuhumu yeyote katika riwaya zake basi atakuwa kamkanusha mwenyezi Mungu na kaibatilisha sheria ya kiislamu" (1)

Na amesema Abuu haatim: "Ametusimulia Harmala akasema: Nimemsikia Imamu Shafi-Mwenyezi Mungu amuwiye radhi- akisema: Sijapata kumuona mtu mwenye kushuhudia uwongo kuliko Raafidhwa".

(1) Rejea: Usuulu Madh-habu Shia Al imaamiyya Al ithna ashariya cha Dr. Naaswir Alqifaary (3/1250)

Na amesema Muammal bin uhaib: "Nilimsikia Yazid bin Haruuna akisema: Inafaa kupokea Hadithi kutoka kwa mtu ambae ni mub-tadii (mzushi) Kama atakuwa hawalingaa nii watu kartu katika bidaa zake, ispokuwa Raafidhwa haifai kupokea kwao kwa sababu ni waongo".

Na amesema Muhammad bin Al asbahany: " Nilimsikia Shariik akisema: chukua elimu kwa kila Mtu utakae kutana nae ispokuwa Raafidhwa usichukue kwake, kwa sababu wao hujiundia hadithi kisha wakaifanya kuwa ni katika Dini".Shariki alietajwa hapo juu ni Sharik bi Abdillahi, aliekuwa kadhwi wa mji wa Kuufa.

Na amesema muaawiya: "Nilimsikia Al-aamashi akisema: "Niliwadiriki watu, ambao walikuwa hawawataji ila kwa sifa ya uwongo".
Anakusudia jamaa zake Mughira bin saidi Raafidhwiy, muongo mkubwa, kama alivyo mtaja al imamu Adh haby (1)

Na amesema Sheikhul Islaam bi taymiyya-mungu amrehemu- katika kuyaelezea waliyo yasema wema walio tangulia kuhusu Raafidhwa: "Ama Raafidhwa asili ya bidaa zao zinatokana na unafiki walio nao pamoja na ukafiri, Uwongo kwao ni mwingi sana, na wao wanakiri hivyo, maana wansema: Hakika Dini yetu ni Taqiyya, ambayo ni mtu kusema kwa ulimi kunyume na yale yaliyomo Moyoni na huu ndio Unafki". (2)

Na amesema Abdallah bin Ahmad bin Ham mbali: "Nilimuuliza Baba yangu kuhusu Raafidhwa, akasema: Ni wale wanao mtukana Abubakari na Omar". Na aliulizwa Imamu Ahmad kuhusu Abubakari na Omar, akasema: "Watakie rehma na ujitenge mbali na kila mwenye kuwachukia." (3) Na amepokea Alkhalaal kutoka kwa Abubakari Al marwazy, amesema: " Nilimuuliza Abuu Abdillah kuhusu wanaomtukana Abubakari na Omar na bibi Aisha, akasema: Sioni kama yuko katika Uislamu mtu huyo".(4)

(1) Rejea: Minhaju sunna cha Sheikhul aislamu bin Taymiyya (1/59-60)
(2) Rejea: Minhaju sunna cha Sheikhul aislamu bin Taymiyya (1/68)
(3) Rejea: Al masaail wa rasaailul-mar-wiyatu an- Ahmad bin Hambali cha abdul-llah bin Sulaiman al-Ahmady (2/357).
(4) Rejea: Assna cha Alkhalaal (3/493). Na hili ni tamko wazi toka kwa Imamu Ahmad kuhusu ukafiri wa Raafidhwa.

Na amepokea Alkhallaal, amesema: "Aliniambia Harbu bin Ismaail Al karmany, Amesema: katuhadithia Musa bin Haruuna bin Zaid, Amesema: Nilimsikia Alfar-yaby akiulizwa na mtu kuhusu hukumu ya mwenye kumtukana Abubakar(r.a), akasem: Ni kafiri, akasema: Inaruhusiwa kumsalia akifa? Akasema: Hapana" (1)

Na ibnu Hazmi-Mungu amrehemu- amesema kuhusu Raafidhwa pindi alipo fanya mdahalo na Manaswara, Wakamletea Vitabu vya Raafidhwa ili wavitumie kujenga hoja: "Hakika Raafishwa sio waislamu, wala kauli zao sio hoja katika Dini yetu, bali hilo ni kundi lililo tokea baada ya kufa mtume (s.a.w) kwa miaka 25, hilo ni kundi linalo pita mapito ya Mayahudi na Manaswara katika ukadhibishaji na ukafiri".(2)

Na amesema Abuu zar-a Arraazy: " pindi ukimuona mtu anamdharau na kumsema vibaya yeyote katika Maswahaba wa Mtume (s.a.w) basi tambua kuwa huyo ni mnafiki".

Na kiliulizwa kitengo cha fat-wa cha Saudi Arabia, anasema muulizaji kuwa yeye na jamaa zake wanaishi jirani na markaz ya kiraki, na kuna kundi la Madhehebu ya Jaafariyya, wamo miongoni mwao waliokataa kula katika vichinjwa vyao, na wengine wakala, sasa swali letu ni kwamba, Je tunaruhusiwa kula katika vichinjwa vyao? Hali ya kuwa wao wanamuomba Ally na Hassani na Hussein na wengineo wakati wanapokuwa na matatizo? Kikajibu kitengo hicho kwa usimamizi wa Sheikh abdul-azizi bin Baz, na Sheikh Abdull razaq Al-afify, na Sheikh Abdallah bin Ghudayaan, na Sheikh abdallah bin Quud. Jawabu lao ni kama ifuatavyo: Kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu peke yake,- na rehma na amani zimfikie Mtume wetu pamoja na Maswahaba zake-.Amma baad:

---

(1)Rejea :Assuna cha Alkhal-llal (3/499)
(2)Rejea : Alfaslu fil milali wa nahli cha ibnu Hazmi(2/78)

Ikiwa hali ni kama alivyo taja muulizaji, kwamba watu anao ishi nao ni kundi la Jaafariya, wanamuomba Ally na Hassan na Hussein,basi ni washirikina na wametoka katika Uislam,na hivyo haifai kula vichinjwa vyao kwa sababu ni mizoga, hata kama watataja jina la Allah katika vichinjwa hivyo.(1)

Na aliulizwa Sheikh Abdallah bin Aljibrin swali, miongoni mwa maelezo aliyo yataja muulizaji: Sheikh katika nchi yetu kuna jamaa mmoja ni Raafidhwa anafanya shughuli ya uchinjaji, hata Ahlu suna wanampelekea wanyama wao awachinje, pia kuna baadhi ya mahoteli wananunua nyama kwake na kwa wengineo katika Raafidhwa wanao fanya kazi kama yake,Je Sheikh, nini hukumu ya vichinjwa vyake?Je ni halali au ni haramu? Tunaomba fat'wa yenu.

Akajibu Sheikh kama ifuatavyo:Waalaykum salaamu warahmatullahi wabarakatuhu.Hayfai huyo Raafidhwa kuwachinja wala kula vichinjwa vyake, kwasababu wao ni washirikina, maana wanamuomba Ally bin Abii Twalib (r.a) wakati wa matatizo hata wakati wa raha, hata wanapo kua Arafa na katika twawafu na sa'ayi, pia wanawaomba watoto wake (Hassan na Hussein) na Maimamu wao, tumewasikiya maranyingi na hii ni shirki kubwa na nikuritadi, na wanastahiki kuuwawa.

Pia wanapetuka mipaka katika kumsifia Ally (r.a) wanamsifu kwa sifa ambazo hazimstahiki yoyote ispokua Allah, tumesikia mara nyingi katika viwanja vya Arafa, kwa vitendo hivyi ni kwamba wametoka katika Uwislam (wameritadi) kwa sababu wamemfanya Ally (r.a) ni Mungu, na ndie mwenye kuuendesha ulimwengu na anajua ghaibu, na sifa nyinginezo.

Pia wanaipinga Qur-ani, wanadai Maswahaba waliibadilisha na wakaondoa baadhi ya aya na sura zinazo wahusu ahlul bayti, na maadui wa ahlul bayti, na hivyo hawaifati, wala hawaioni kama ni dalili.

Vilevile wanawatukana na kuwataja vibaya Maswahaba wakubwa kama vile makhalifa watatu,na Maswahaba kumi walio bashiriwa pepo na Mtume (s.a.w),pia wakezake Mtume (s.a.w) ambao ni mama wa waumini, na Maswahaba mashuhuri kama Anasi, Jaabir, Abu huraira na wengineo, hawazikubali Hadithi zao kwa sababu wanasema ni makafiri!! Wala hawazikubali Hadithi zilizopo katika sahihi mbili (Bukhari na Muslim) ispokua zinazo wazungumzia ahalul-bayti, badala yake wanashikamana na Hadithi za uongo ambazo hazina dalili yoyote juu ya madai yao, pia pamoja na hayo wao wanatumia unafiki kwa kusema kwa

ndimi zao yalio tafauti na walio yaficha nyoyoni mwao, na wanasema "Asiye kuwa na Taqiya hana dini". Hivyo madai yao yakua ni ndugu zetu katika imani, na kwamba wanaipenda dini ni madai ya uongo ya siyo kubalika. Tunamuomba Allah atukinge na shari zao.Rehma na Amani zimfikie Mtume (s.a.w) pamoja na Ahli zake na Maswahaba wake.(1)

(1) Fat'wa hii ilitolewa na Sheikh baada ya kuulizwa swali kuhusu kushirikiyana na Raafidhwa ilikua ni mwaka 1414 H. Pia na panda kubainisha kuhusu maneno ya semwayo na baadhi ya watu kuwa Sheikh Jibrin pekeyake ndio kawakufurisha Raafidhwa, maneno haya si kweli, bali wema walio tangulia wote walilikufurisha kundi hili.

*SURATUL-WILAYA AMBAYO WANADAI ILIONDOLEWA KATIKA MAS-HAFU:*

Imenukuliwa kutoka katika kitabu (faslul-khitwaab). "Enyi mlio amani ziaminini nuru mbili tulizo ziteremsha, zikikusomeeni aya zangu na kukutahadharisheni na adhabu ya siku kubwa. Nuru mbili hizi, moja yatokana na nyingine, na mimi ni mwenye kusikia na mjuzi. Hakika wale wanao tekeleza ahadi zao, pamoja na Mtume wake katika aya zangu wataingia katika Pepo yenye neema. Na wale walio kufuru baada ya kuamini kwao kwa kuzitenga ahadi zao, na yale aliyo wataka Mtume wayafuate, basi watatupwa katika moto wa Jahimu. Walizidhulumu nafsi zao na wakamuasi yule alie muusia Mtume basi hao watanyweshwa motoni maji yachemkayo hakika Mwenyezi mungu ambae kaitia nuru mbingu na ardhi kwa alivyo taka, na akawachagua baadhi ya Malaika, na akajalia waumini miongoni mwa viumbe wake,na Mwenyezi Mungu anafanya ayatakayo, hakuna Mola mwingine isipokua yeye, mwingi wa rehma mwenye kurehemu. Kwa hakika walifanya vitimbi walio kuwa kabla yao kwa Mitume wao, basi Mwenyezi Mungu akawatia mikononi kwa sababu ya vitimbi vyao, hakika ukamataji wangu ni mkali na wenye kuumiza. Hakika Mwenyezi Mungu aliwaangamiza watu Aad na Thamud kwa ajili ya yale waliyo yachuma, na akawafanya ni mazingatio kwenu, je hamuogopi?. Na Firauni kamuangamiza kwa ujeuri wake kwa Mussa na ndugu yake Haruna, nikamzamisha baharini na wafuasi wake wote. Ili iwe ni mazingatio kwenu na hakika wengi wenu ni waovu. Hakika Mwenyezi Mungu atawajumuisha hiyo siku ya kukusanywa, hawataweza kujibu lolote pindi watakapo ulizwa. Hakika moto wa Jahimu ndio makazi yao na Mwenyezi Mungu ni mjuzi mwenye hekima. Ewe Mtume wafikishie uwonyaji wangu, Hivi karibuni watajua. Kwa hakika wamepata hasara wale waliokuwa wakizipinga aya zangu na hukumu zangu. Mfano wa wale wanaotelekeza ahadi zao, hakika nitawalipa Pepo yenye neema. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye maghfira na malipo makubwa. Hakika Ally ni katika wacha mungu. Na hakika sisi tutampa haki yake siku ya Qiyama.

Hatukuwa sisi juu ya dhulma aliyofanyiwa ni wenye kughafilika. Na tulimkirimu juu ya watu wako wote. Hakika yeye na kizazi chake ni wenye subira. Na hakika adui yao ni kiongozi wa waovu sema uwaambie walio kufuru baada ya imani yao mmetafuta mapambo ya dunia na mmeyafanyia haraka mkasahau aliyokuahidini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mkazitengua ahadi baada ya kuahidi kwenu, na tumekupigieni mfano huenda mkaongoka. Ewe Mtume kwa hakika tumekuteremshia dalili zenye kupambanua mna ndani yake kwamba atakaefishwa ili hali ni Muumini, na watakao mtii baada yao watadhihiri.

Basi jiepushe nao hakika wao wamekengeuka. Kwa hakika sisi tutawahudhurisha, katika siku ambayo hakitawasaidia chochote wala hawata hurumiwa. Wataingia katika jahannam makazi ambayo hawataondolewa. Basi litukuze jina la Mola na uwe ni miongoni mwa wenye kusujudu. Hakika tulimpeleka Mussa na Haruna wakawakanusha. Wakavumilia juu ya kukadhibishwa huko. Tukawageuza-wakadhibishaji-kuwa Manyani na Ngurue na tukawalani mpaka siku ya mwisho. Basi subiri hivi karibuni wataona. Kwa hakika tumekupa hukumu kama zile tulizo wapa wale wa kabla yako miongoni mwa mitume na tukakuchagulia miongoni mwao mteule ili wapate kurejea. Na yeyote atakae kengeuka amri yangu, basi kwangu ndio marejea yake, Basi na wastarehe kidogo na ukafiri wao, wala usiulize kuhusu wale wenye kuvunja ahadi. Ewe Mtume hakika tumeweka katika shingo za waumini ahadi, basi ichukue na uwe miongoni mwa wenye kushukuru. Hakika Ally ni mnyenyekevu, mwenye kusimama sana usiku akiogopa akhera na kutaraji thawabu za Mola wake, sema: jee wako sawa wale walio dhulumu hali ya kuwa wanazitambua adhabu zangu? Tutaweka shingoni mwao makongwa, nao watajuta juu ya matendo yao. Hakika sisi tumekubashiria kizazi chake chema. Na wao hawatazikhalifu amri zetu. Wanazo rehma kutoka kwangu katika uhai wao na katika kufa kwao na siku ya kufufuliwa wale wanaowafanyia uwadui baada yako wanazo ghadhabu zangu, hakika hao ni watu waovu waliopata khasara. Na wale waliopita mapito yao wana rehma toka kwangu nao watakuwa katika vyumba vya Peponi katika hali ya amani kabisa. Na shukuruani zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote.(1)

(1) Hii ndio Suuratul'wilaya wanayodai Mashi,imenukuliwa kutoka katika kitabu Faslul-khitwaab fii ithbat takhriif kitaabil rabil arbaab, tumeamua kuiandika ili msomaji aweze kuona jinsi wanavyomkanusha Allah ambae kahidi kukilinda kitabu chake kutokana na kubadilishwa.

## *LAUHU (UBAO) WA FAATWIMA WANAO DAI MASHIA*

Hiki ni kitabu kutoka kwa mwenyezi Mungu mtukufu mwnye hekma kwa Muhmmad nabii wake na nuru yake na mjumbe na dalili yake, ambacho kateremka nacho Jibrilu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ewe Muhammad yatukuze majina yangu, na uzishukuru neema zangu, wala usikanushe utukuufu wangu, hakika mimi ndio Mola wako hapana Mola wa haki ila mimi, basi atakae tegemea fadhila zisizokuwa zangu, au akaogopa usiokuwa uadilifu wangu, basi nitamuadhibu adhabu ambayo sitomuadhibu yoyote katika walimwengu wote, basi niabudu mimi, na unitegemee mimi tu, hakika mimi sijapata kumtuma Nabii yeyote akakamilisha masiku yake na kumaliza muda wake isipokuwa huwa ninamjalia waswiy(mrithi), na mimi nimekufadhilisha juu ya manabii wote na nimemfadhilisha (mrithi wako) juu ya warithi wote , na nimekukirimu kwa wajukuu zako wawili, nikamjalia Hassan kuwa ndio madini ya elimu yangu baada ya kumalizika muda wa baba yake. Na nikamjali Hussein kuwa ni hazina ya wahyi wangu, na nikamkirimu kwa kufa shahid na nikafanya mwisho wake ni mwema, yeye ni mmbora wa mashahidi na mwenye daraja kubwa. Nikajaalia neno langu na hoja yangu kwake, kwa sababu ya kizazi chake ninaadhibu na kulipa mema, wa mwanzo wao ni Ally ambae ni bwana wa Wacha mungu na pambo la wateule wangu, na mwanae ni sawa na babu yake mwenye kusifiwa Muhammad Al baakir. Wataangamia wenye kutia shaka juu ya Jaafari, Mwenye kumkanusha ni sawa na alie nikanusha mimi. Limekwisha thibiti neno langu kuwa nitayakirimu makazi ya Jaafari. Mwenye kubadilisha aya moja katika kitabu changu basi atakuwa kanizuliya. Ole wao wazushi wakanushao, Pindi ukimalizika muda wa mussa mja wangu na kipenzi changu na mmbora wangu kwa Ally(…..) (1) Atazikwa katika mji ambao kaujenga mja mwema, kandokando ya mtu mmbaya kabisa katika viumbe vyangu. Limekwisha timia neno langu kwa Muhammad mwanae na khalifa wake baada yake na mrthi wa elimu yake.

(1) Hapa kuna ibara haikuwa wazi hivyo hatukuiandika ibara hiyo.

Yeye ndie mrithi wa elimu yangu na ndie hoja yangu kwa viumbe wangu, hato muamini mja yoyote isipokuwa nitayafanya makazi yake ni Peponi na nitampa nafasi ya uombezi wa watu sabini katika watu wa nyumbani kwake ambao wote walistahiki kuingia motoni, na nitampa mwisho mwema mwanae Ally kipenzi changu, na muaminifu juu ya wahyi (ufunuo) wangu. Nitamtoa kwake mlinganiaji katika njia yangu na mlinzi wa elimu yangu Alhassan na nilikamilisha hilo kwa mwanae (….) (1) Rehma kwa walimwengu, atakuwa na ukamilifi wa Mussa na uzuri wa Issa na subira ya Ayubu, watadhalilishwa Mawalii wangu katika zama zake, na watauwawa na kuchomwa moto, na watakuwa wenye khofu na uwoga, Ardhi itatapakaa Damu yao, na kuenea hali ya hatari kwa wake zao hao ndio mawalii wangu wa kweli, kupitia kwao nitiondoa fitna, na kwao nitaondoa matatizo na misukosuko, hao ndio wana Rehma na Amani kutoka kwa Mola wao na hao ndio wenye kuongoka.

Kasema: Abdurrahmani bin Saalim: amesema Abu Baswiir: lau kama hutasikia maisha yako yote ispokuwa hadithi hii basi inakutosha, hivyo ihifadhi ispokuwa kwa watu wake. (2) (3)

(1) Kuna ibara ambayo haiko wazi ndio mana hatukuweza kuiandika.
(2) Raafidhwa wanadai kuwa ubao wa Faatwima alishuka nao Jibriilu (a.s) kwa Faatwima- Allah amuwiye radhi-baada ya kufa Mtume (s.a.w), na kwamba Ally (r.a) wakati Jibrilu akishuka kwa Faatwima alikuwa kajificha nyuma ya pazia akawa anaandika ayasemayo Jibrilu kumwambia Faatwima.(kama alivyoeleza Alkulayny katika kitabu chake Alkaafii(1/185-186) na huu ni uwongo na uzushi mkubwa, maana wahyi ulikatika baada ya kufa mtuma (s.a.w), pamoja na hayo ubao huwo wanao udai kwao ni sawa na Qur-ani tukufu kwa Ahlu Sunna.
(3) Rejea: alkaafii cha Alkulayny (1/527), na Alwaafii cha Alfaidhu Alkaashrany juzuu ya kwanza (2/72) na Ikmaalu ddiin cha Ibnubabawahi Alqummy uk.301-304, na I-ilaamul-waraa cha Abii Ally Attwabrasy uk.152.

*DUA YA MASANAMU WAWILI WAKIKURAISHI (1) WANAMKUSUDIA ABUBAKARI NA UMAR MUNGU AWAWIYE RADHI.*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma Mwenye kurehemu.

Ewe Mwenyezi Mungu, mpe rehma na amani Muhammadi na watu wake, ewe Mwenyezi Mungu walaani masanamu wawili wa kikuraishi na matwaghuti wao na mabinti wao, ambao walikhalifu amri yako, na wakaukanusha wahyi wako, na wakazikanusha neema zako, na wakamuasi Mtume wako, na wakageuza dini yako, na wakakibadilisha kitabu chako, na wakawapenda maadui zako, na wakazipindisha hukumu zako, na kuzigeuza aya zako, na wakawafanyia uadui mawalii wako, na wakauharibu mji wako na kuwaharibu waja wako.

Ewe Mwenyezi Mungu walaani, na wafuasi wao, na wenye kuwapenda, kwa hakika waliiharibu nyumba ya utume, na wakavunja mlango wake, na kuharibu sakafu yake, na kuwaondoa watu na wakauwa watoto wake, na wakaiepusha mimbari yake na mrithi wa elimu yake, na wakakanusha uimamu wake, na wakamshirikisha Mola wao, yakawa makubwa madhambi yao, na kwa hiyo wakawa ni watu wa kudumu motoni, na kipi kitakujulisha hiyo saqar? Haibakishi wala haisazi.

Ewe Mwenyezi Mungu, walaani kwa idadi ya kila ovu walilo lifanya, na kwa kila haki waliyo ificha, na kwa kila mimbari walioipanda, na kwa kila mnafiki walio mtawalisha, na kwakila walio muudhi, na kwakila mkweli walie mfukuza,na kwakila kafiri walie mnusuru, na kila kiongozi walie mtenza nguvu, na kila faradhi waliyoibadilisha, na kila athari walio ibadilisha, na kila damu walio imwaga, na kwakila kheri waliyo ibadilisha, na kila ukafiri walio usimamisha, na kila haramu walio ila na kila khumus walio jihalalishia na kila batili walio iasisi na kila unafiki walio uficha, na kila dhulma walio ieneza, na kila amana walio ifanyia khiyana, na kila ahadi walio ivunja, na kila halali walio iharamisha, na haramu walio ihalalisha, na kila mtukufu walio mdhalilisha, na kila dhalili walio mtukuza….

(1) Tumeamua kuikopi dua hii ambayo wanaiita dua ya masanamu wawili wa kikuraishi, ili msomaji aweze kuisoma ambayo wanamkusudia Abubakari na Umar na Bibi Aisha na Bi Hafswa Mwenyezi mungu awawiye radhi wote.

Ewe mwenyezi mungu, walaani kwa idadi ya kila aya waliyo ibadilisha, na kila faradhi walio iacha, na kila sunna walio ibadilisha, na kila hukumu walio ivunja, na kila wasia walio ubadilisha, na kila mambo waliyo yabadilisha, na mambo waliyoyapoteza, na kila shahada walizo zificha na kila khiyana waliyo ifanya.

Ewe Mwenyezi Mungu walaani katika siri na dhahiri, laana zilizokuwa nyingi kabisa, daima isiyo na kikomo, laana isiyo malizika, walaani wao na wasaidizi wao, na kila mwenye kuwapenda, na kila wenye kufuata maneno yao na wenye kuzisadikisha hukumu zao.

(Kisha sema mara nne) Ewe Mwenyezi Mungu walaani wote, ewe mola mpe rehma Mtume (s.a.w) pamoja na Ahli zake, nitosheleze kwa halali zako kutokana na haramu zako, na unikinge na ukafiri. Ewe Mola wangu hakika nimekosea na kuidhulumu nafsi yangu, ninakiri madhambi yangu na sasa niko mbele yako iweke nafsi yangu katika radhi zako, sitorejea, na kama nikirejea basi nisamehe, kwa fadhila na ukarimu wako, ewe mwingi wa huruma. Rehma na amani zimfikie bwana wa Mitume na mwisho wa manabii wote na Ahli zake watukufu, ewe mwingi wa rehma".(1)

(1) Rejea: Miftaahul-jinaan cha Abbas alqummy uk.114

## *HITIMISHO*

Baada ya yote yaliyotangulia, bila shaka ndugu yangu Muislamu utakubaliana na mimi kwamba mwenye kuifuata dini hii potofu si miongoni mwa Waislamu hata kama yeye atajiita Muislamu,sasa nini wajibu wako wewe ndugu yangu Muislam juu ya hawa Raafidhwa hasa ukizingatia kuwa wanaishi na Waislamu na wanajinasibisha na Uislamu?

Wajibu wako ni kuchukua tahadhari nao, na kutoshirikiana nao na kuwatahadharisha watu kutokana na itikadi zao mbaya ambazo zimejengeka juu ya kumfanyia uadui kila mwenye kumpwekesha Allah na kumuamini Allah na Mtume wake (s.a.w).

Ameema Sheikhl islaam bin Taymiyya: " Ama Raafidhwa hawaishi na mtu yeyote ispokuwa katika misingi ya unafiki kwa sababu dini yao iliyomo nyoyoni mwao ni mbovu, inawafanya waishi katika misingi ya uwongo na khiyana, na kuwafanyia watu ubaya, hawaachi shari yoyote walio na uwezo nayo isipokuwa huifanya. Na endapo wakiwa hawajulikani kwa watu kuwa ni Raafidhwa basi utaona nyusoni mwao alama za unafiki" (1)

Hakika wao wameficha chuki nyingi dhidi yetu, pamoja na hivyo utawaona baadhi ya watu katika Ahlu sunna wenye kudanganyika nao wanashirikiana nao na kuwaamini sana, na yote hii ni kwasababu ya kuwa mbali na kitabu cha Allah na kuyapa nyongo mafundisho ya dini yetu na kutojua hukumu zake zinazo muamuru muislamu kujiweka mbali na kila kafiri na mshirikina. Kwa maelezo haya bila shaka tutakuwa tumejua wajibu wetu kama waislamu.

Tunamuomba Allah ainusuri dini yake, na alinyanyue neno lake, na awadhalilishe Raafidhwa na wafuasi wao, na awafanye kuwa ni ngawira kwa waislamu. Rehema na amani zimuendee Mtume Wetu (s.a.w) na Ahli zake na Maswahaba zake wote.

Imeandikwa na Abdallah bin Muhammad Assalafy. Mwenyezi Mungu amsamehe yeye na wazazi wake na Waislamu wote.

---

(1) Rejea: Minhaaju sunnati annabawiyya cha Sheikhul Islaam ibni Taymiyya (3/360)

## *REJEA MUHIMU AMBAZO TUNAMNASIHI KILA MUISLAMU KUZIJUA KATIKA KUWAJIBU RAAFIDHWA*

1-Fatawa Sheikhl Islaamu bin Taymiyya
2-Minhaju Sunna cha Sheikhl Islaamu bin Taymiyya
3-Almilal wa nnihal cha Ashaharistany
4-Alfarku baynal firaq cha Al bghadaady
5-Maqaalatul-Islaamiyyiin cha Al ash-ary

Miongoni mwa vitabu vya wanazuoni wa zama hizi

1-Vitabu vyote vya Sheikh Ihsan ilahi dhwahir
2-Mas'alatu taqriib cha Sheikh d.r Naaswir Alqifar
3-Usuul Madh'habu Shia Al ithna ashariya cha Sheikh Naaswir Alqifar
4-Vitabu vyote vya Shekh Muhammad Maali Llahu
5-Badhlul-majhuud fii mushaabahat Raafidhwa lil yahuudi cha Abdalla Aljamily.
6-Hattaa laa nan khadi'a cha Abdalla Al muuswily
7-(Ashi'atul Ithnaa'ashariya watakfiirihim liumuumil muslimiin) cha Abdallah Assalafy
8-(Man qatalal'Hussein) cha Abdallah bi Abdul Aziiz
9-(Alburhani fii tabriat abi Huraira minal buhtani) cha Abdallh Annaaswir
10-(Al intiswaar lisuhbi wal aal) cha Ibrahiim Arrahiily
11-Kashfu ljaany Muhammadut-tijaaniy) cha Sheikh Uthman Alkhamis
12-(Bal dhwalaltu fii radd abaatwiil at-tijaany) cha Sheikh khaalid Al Asqalaany
13-(Ma'al Ithnaa'ashariya fil usuul walfuruu) cha Dr. Ally Assaaluus
14(Tabdiidu dhwalaam watambiihu niyaam alaa khatwari tashayyui ala lmuslimiin wal islaam) cha Sheikh Sulaimaan Aljabhan. Na vingine vingi tu.

*TOVUTI MUHIMU ZA KUWAJIBU RAAFIDWA ITHNAA ASHARIYA, AMBAZO TUNAKUSIHI UZITEMBELEE*

1- http://www.dd-sunnah.net
2-http://www.fnoor.com
3-http://www.albrhan.com
4-http://www.wylsh.com
5-http://www.khomainy.com
6-http://www.dhr12.com
7-http://www.albainah.net
8-http://www.ansar.org
9-http://www.almanhaj.com
10-http://www.isl.org.uk
11-http://www.almhdi.com

*YALIYOMO:*


| Maudhui . | Ukurasa. |
| --- | --- |
| Utangulizi wa Sheikh ibn Bazi…………………………….. | 1 |
| Utangulizi……………………. | 2 |
| Lini wamedhihiri?............................ | 3-4 |
| Kwa nini Shia wameitwa Raafidhwa?........................... | 5 |
| Raafidhwa wamegawanyika makundi mangapi?......................... | 6 |
| Ni ipi itikadi ya (Albadaa) wanayo iamini Raafidhwa?...................... | 7 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu sifa za Allah?....................... | 8-9 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu Qur-ani tuliyo nayo aliyo ahidi Allah kuilinda?....... | 10-12 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa juu ya Maswahaba wa Mtume?.................... | 13-16 |
| Raafidhwa wanafanana vipi na Mayahudi?............................... | 17 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu Maimamu?............................... | 18-19 |
| Ni ipi itikadi ya kurejea wanayo iamini Raafidhwa?........................... | 20-21 |
| Ni ipi itikadi ya Taqiyya kwa Raafidhwa?.................................. | 22-23 |
| Ni ipi itikadi ya udongo waliyo nayo Raafidhwa?.............................. | 24 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu Ahlusuna?................................... | 25-26 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu Mut'a na ina ubora gani?.................... | 27-29 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu Najaf na Karbala na zinaubora gain?........................................... | 30- 32 |
| Raafidhwa wanatofautiana na Ahlusuna katika mambo gain?..................... | 33 |
| Ni ipi itikadi ya Raafidhwa kuhusu Ashuraa na inaubora gani?.................. | 34 |
| Ni ipi itakadi ya Raafidhwa kuhusu Albay'a?.................................... | 35- 36 |
| Ni ipi hukmu ya kujenga mahusiano baina ya Raafidhwa na Ahlusuna?....... | 37 |
| Maneno ya wema walio pita kuhusu Raafidhwa…………………. | 38- 42 |
| Suratul wilaya waliyo idai Mashia………………………………… | 43- 44 |
| Ubao wa Fatma walio udai Mashia………………………………… | 45- 46 |
| Dua ya masanamu wawili wa kikuraishi(Abubakari na Omar)…… | 47- 48 |
| Hitimisho…………………………………………… | 49 |
| Rejea muhimu za kuwajibu Mashia…………………………………… | 50 |
| Tovuti muhimu za kuwajibu Raafidhwa ithna asharia……………… | 51 |
| Yaliyomo | 52 |